epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumatatu Agosti 5, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581759

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

GUARDIOLA AJIBU UVUMI WA KUINOA ENGLAND



Msemaji wa Jeshi la Polisi, DCP David Misime

# Adaiwa kuwatuma askari kubaka binti

• **Waziri**, wanaharakati wang'aka; Polisi yasema inasaka wahusika...*Endelea ukurasa 2*



Dk. Dorothy Gwajima



Ananilea Nkya



Boniface Jacob

UKURASA WA 7

**MBUNGE ATIMULIWA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI, DC AINGILIA KATI**

UKURASA WA 8


**AJALI YA MALORI ILIVYOKATISHA UHAI WA MMILIKI MABASI YA SAULI**

UKURASA WA 15

**NIDHAMU YAPONZA VIJANA, WANAWAKE SEKTA YA KILIMO**

## Zitto 'alia' kuzuiwa kukutana na raia 162,000 wizara yamjibu

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Mwalimu wake aliyemfundisha Chuo cha IDM Mzumbe (Sasa Chuo Kikuu Mzumbe) Mwl.Sabina Geleja (kulia) na aliyekuwa mwanafunzi mwenzake Dk Stella Kinemo mara baada ya hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa Kampasi mpya ya Chuo Kikuu Mzumbe jana. **PICHA: IKULU**

# Samia awapa jukumu maalum Bashe, Jafo uzalishaji sukari

UK. 3

**MICHEZO** **WANANCHIII, BIASHARA KAMILI NGAO YA JAMII** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Adaiwa kuwatuma askari kubaka binti

**Na Mwandishi Wetu**



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima




Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna David Misime,

BINTI ambaye umri wake haujatajwa, mkazi wa Mtaa wa Msakala na Dovya, jirani na Shule ya Msingi Yombo Dovya, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam, anadaiwa kubakwa na kulawitiwa na vijana watano ambao wanadaiwa ni askari wa moja ya vikosi vya ulinzi nchini.

Vijana hao walimpiga picha mjongeo wakati wanamfanyia ukatili huo binti huyo kisha kuisambaza katika mitandao ya kijamii, wakidaiwa kutumwa na bosi wao aliyedai kuwa binti huyo ana uhusiano wa kimapenzi na mumewe.

Tukio hilo liliibuliwa na aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob ambaye aliandika mkasa mzima kwenye ukurasa wake wa X huku akiwatumia nakala (tag) Rais Samia Suluhu Hassan kama Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi Tanzania, Waziri wa Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Stergomena Tax na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima.

Meya Boniface aliandika: "Binti huyu amebakwa na kulawitiwa akiwa anarekodiwa video tatu tofauti. Askari hao walimrekodi wakiwa wanambaka na kumlawiti, wamesambaza video zake mitandaoni kwa maagizo ya kiongozi wao (afande) ambaye amewatuma kumpatia huyu binti adhabu.

"Kwa maelezo ya vijana hao (askari), kosa la huyu binti ni kutembea na mume wa bosi wao (afande), Mahojiano katika video hizo tatu tofauti yanaonesha binti amekamatwa na kubakwa na kulawitiwa nje ya Mkoa wa Dar es Salaam," alidai Jacob.

Anadai kuwa afande huyo aligundua kuwa mume wake ana uhusiano na binti huyo kupitia ujumbe mfupi wa maandishi waliokuwa wanawasiliana, ndipo alichukua simu ya mume wake na kuendelea kuwasiliana na binti kwa ujumbe wa kimapenzi.

Meya huyo wa zamani anadai kuwa mwanamke huyo aliwasiliana na binti huyo na kukubaliana kukutana na kumtumia fedha za nauli ndipo binti alichukua usafiri kwenda alikoelekezwa na alipofika, aliwasiliana na mwenyeji wake ambaye alimwelekeza aliko na alipofika, alipokewa na vijana hao kisha kupelekwa eneo walikomtenda ukatili huo.

Meya huyo mstaafu anaendelea kudai kuwa: "Sisi Watanzania tuliohuzunishwa na ukatili huu, tunataka kuona vijana wote watano na kiongozi aliyewatuma wanakamatwa na kufikishwa mbele ya mkono wa sheria.

"Kuona majeshi yetu yenye heshima kubwa sana barani Afrika, yanajitenga na kashfa hii ya ubakaji kwa raia wake. Majeshi na vikosi vyote vinafanya msako na utambuzi wa watu hawa, kisha wawakabidhi katika vyombo vya kisheria na kushtakiwa kama kweli ni waajiriwa wa majeshi yetu.

"Kwa kuwa Amiri jeshi Mkuu wa Majeshi ya Tanzania ni mama, Waziri wa Ulinzi ni mama, Waziri wa Wanawake ni mama, tunatarajia kuona wakichukizwa zaidi juu ya udhalilishaji na ukatili juu ya mtoto wa kike wao wakiwa kama wazazi na viongozi wenye dhamana ya kulinda raia wa Tanzania," Jacob anasema.

**JESHI LA POLISI**

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna David Misime, jeshi hilo linafanyia kazi taarifa za tukio hilo.

"Kwenye mitandao ya kijamii inaonekana video inayosambazwa ikimwonesha binti anayesemekana ametokea Yombo Dovya, Jiji la Dar es Salaam akidhalilishwa na kufanyiwa ukatili ambao haukubaliki kwani ni kinyume cha sheria, maadili ya Mtanzania na haki za binadamu," Naibu Kamishna huyo alisema katika taarifa yake hiyo.

Naibu Kamishna Misime alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kuacha kuendelea kusambaza video hiyo kwa kuwa kusambaza ni kosa kisheria, pia ni kuendelea kudhalilisha utu wa binadamu.

"Pia tunatoa wito kwa mwenye taarifa ya kuhakikisha mkono wa sheria unawafikia kwa haraka waliofanya ukatili huu, asisite kutusaidia kwa kutupa taarifa au kumpatia kiongozi yeyote yule wanayemwamini kwamba taarifa ikimfikia watu hao watapatikana haraka iwezekanavyo au toa taarifa kupitia namba 0699998899," alisema.

**WAZIRI GWAJIMA**

Katika ujumbe huo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima aliandika jana: "Ahsante sana kunaTag. Nimesoma na kuwasilisha kwenye mamlaka yenye dhamana ya kuchunguza na kukamata ambayo ni Wizara ya Mambo ya Ndani. Watatoa taarifa kwa nafasi yao.

"Kwa namna yoyote ile, taarifa hii inasikitisha na jambo kama hili halifai, ni la kulaaniwa na haliwezi kufumbiwa macho. Iwapo manusura au aliyekaribu naye atasoma hizi taarifa, wasiogope, watoe taarifa ili manusura apate msaada haraka, ikiwamo huduma za afya, kisaikolojia na usalama.

"Namba zetu ziko hewani, yangu mwenyewe ni... (akataja namba zake za simu) na za wizara ziko kwenye tangazo letu.

"Aidha, tuvipe ushirikiano vyombo vyetu kila mwenye taarifa namba za IGP alizotangaza ni... (akataja namba za simu). Asanteni, tuendelee kushirikiana kulinda jamii yetu. Sisi ni jamii moja, uovu hapana!"

Waziri Dorothy pia alisema akiambatanisha taarifa ya Jeshi la Polisi kwenye ukurasa wake na kuandika: "Kwa kurejea taarifa ya Jeshi la Polisi, ndugu wanajamii, tuendelee kutoa ushirikiano sasa na daima. Asanteni sana, Asanteni sana."

Baada ya ujumbe huo, wananchi waliendelea kuandika ujumbe, wakimpongeza kwa kuwa na utaratibu wa kufanyia kazi haraka taarifa anazopewa.

"Wewe mama (Gwajima) ni mtu makini sana kati ya mawaziri tulionao. Hili jambo si la kuachiwa raia tupige kelele wenyewe. Kila mpendahaki anapaswa kupaza sauti. Mungu akuongezee maarifa na hekima," aliandika mmoja wa waliosoma ujumbe wa waziri huyo.

**WANAHARAKATI**

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema wanalaani tukio hilo huku wakieleza kuongezeka matukio ya vyombo vya ulinzi kujichukulia sheria mkononi panapotokea tofauti baina yao na raia.

Alisema ni muhimu kukawa na mwongozo kwamba waache kutumia vibaya madaraka yao kwa kuwa hakuna aliye juu ya sheria na inapotokea wamekosana na raia, zifuatwe taratibu na si kutumia nguvu na kuumiza raia, jambo linalosababisha utawala wa sheria kutoheshimiwa.

"Tunapokea malalamiko mengi ya kundi hili kuwatendea ubaya raia, kukiwa na mgogoro wa ardhi, hivi karibuni kuna tukio la askari huko Mkuranga alihisi raia anatembea na mkewe, alikusanya wenzake wakakamata raia wakawapiga, lakini kuna tukio la mwanajeshi kumpiga dereva wa daladala.

"Ni muhimu viongozi wakakemea vikali haya matukio haya kuondoa dhana kwamba mtu akiwa mwanajeshi/askari anaweza kufanya jambo lolote kwamba wako juu ya sheria. Tunataka wahusika wa tukio hili wakamatwe na wafikishwe kwenye mahakama kwa uwazi na si usiri," alisema.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Ananilea Nkya, alisema waliotenda tukio hilo wamekiuka Sheria ya Kudhibiti Makosa ya Kujamiiana ya Mwaka 1998, hivyo lazima polisi wawakamate kisha wapelekwe mahakamani ili haki ipatikane.

"Hakuna mtu aliye juu ya sheria, hakuna sababu yoyote kwa Jeshi la Polisi kuogopa kumkamata yeyote aliyetenda ukatili huo, kila mmoja ana wajibu wake na hivyo lazima sheria ziheshimiwe na hatua kali zichukuliwe mara moja na kuwafikisha mahakamani.

"Hakuna sababu yoyote inayohalalisha mtu kubakwa. Kubaka mtu ni kosa la jinai, jinai ikitendeka lazima hatua zichukuliwe. Hatua zisipochukuliwa itaonyesha kuna watu wako juu ya sheria, jambo ambalo ni hatari sana kwa nchi yetu," alisema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia tukio hilo, alisema:

"Inasikitisha kuwa wanaotakiwa kulinda haki ndiyo wanavunja haki. Jambo hili si tu ni jinai, bali pia ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

"Kama mume amechepuka, kuna Sheria ya Ndoa (1971), hivyo angeomba talaka au kumsamehe, na si kumfanyia ukatili. Habari hii ikithibitika, wote wachukuliwe hatua za kisheria maana hakuna aliye juu ya sheria. Tutaifuatilia kesho (leo) ili tumpe huyu binti msaada wa kisheria."

HABARI KITAIFA



Ofisa Mawasiliano Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Semu Mwakyanjala (kulia), akitoa maelezo ya fursa zilizopo katika sekta ya mawasiliano nchini kwa raia wa China aliyetembelea Banda la mamlaka hiyo jana kwenye Maonesho ya Nanenane yanayoendelea jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia awapa jukumu maalum Bashe na Jafo uzalishaji sukari

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo kuanza mchakato wa mabadiliko ya sera ili viwanda vya sukari vya ndani viwe na uwezo wa kuzalisha sukari ya viwandani na malighafi ya kuzalisha nishati safi ya kupikia na matumizi mengine.

Vilevile, Rais ameagiza Chuo Kikuu cha Mzumbe kurejesha utaratibu wa kufundisha viongozi wa serikali ili kuongeza uwajibikaji na kupata watumishi wanaotekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Rais Samia aliagiza hayo jana kwa nyakati tofauti wakati akizungumza na wananchi katika ziara yake mkoani Morogoro baada ya kufungua mradi wa ujenzi wa barabara ya Kidatu-Ifakara yenye urefu wa kilometa 66.9 na daraja la Mto Ruaha Mkuu, kuweka jiwe la msingi wa ujenzi wa jengo la Chuo Kikuu cha Mzumbe na kufungua mradi wa upanuzi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero.

Alisema kama viwanda vya sukari vya ndani vikizalisha sukari ya viwandani, vitaipunguzia serikali matumizi ya fedha za kigeni kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi na hivyo kusaidia kukabili uhaba wa dola nchini.

Alisema mahitaji ya sukari ya nyumbani ni tani 650,000 huku ya viwandani ikiwa ni tani 250,000 na kwamba kuendelea kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi ni matumizi mabaya ya fedha za kigeni.

"Nina uhakika tukivipa kazi viwanda vyetu vinaweza kutuzalishia sukari ya viwandani na hiyo sasa ndio kazi ninayotaka mkaifanyie kazi, angalieni mtawekaje sera zetu ili viwanda hivi vizalishe sukari ya viwandani, lakini pia wazalishe 'Ethanol' kwa ajili ya kupata nishati safi ya kupikia na viwanda vingine," aliagiza.

Rais alimwagiza Waziri wa Kilimo (Bashe) kujadiliana na wazalishaji sukari changamoto zilizopo kwa upana na kuzitatua ili kuwawekea mazingira mazuri ya uzalishaji, lengo likiwa ni kuhakikisha nchi inajitosheleza kwa chakula.

Rais Samia alisema serikali ipo tayari kubadilisha sera na sheria za nchi ili kuweka mazingira mazuri ya wawekezaji, lengo likiwa kujihakikishia uzalishwaji chakula cha kutosha kwa mahitaji ya ndani na nje.

Akiwa katika Jimbo la Mikumi, Rais alishauri wananchi wa eneo hilo kuwekeza katika nyumba za wageni ili kujiongezea kipato kutokana na ongezeko la watalii linalosababishwa na matangazo aliyoyafanya kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour pamoja na treni ya kisasa ya mwendokasi.

Rais pia alisema serikali imetenga Sh. bilioni 7.2 kwa ajili ya kuendeleza Bonde Ruhembe, fedha hizo zitatumika kufanya utafiti, kujenga mabwawa kwa ajili shughuli za kilimo ikiwamo mpunga na miwa na kujenga kingo zitakazodhibiti mafuriko.

Alisema itendelea kuwapa wakulima ruzuku ya mbolea na inajipanga kwa ajili ya kuwapa ruzuku za mbegu, ili kupunguza changamoto zitokanazo na uzalishaji mazao ili nao wafurahie matunda ya kazi zao.

Alipongeza Watanzania kwa kazi nzuri ya kuongeza uzalishaji chakula kwa kuwa kwa mara ya kwanza mwaka huu nchi imeuza tani milioni 1.1 za chakula Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na tani 600,000 zimeuzwa Zambia.

Akiwa Mzumbe, Rais aliagiza chuo kikuu hicho kurejesha utaratibu wa kufundisha viongozi wa serikali ili kuzalisha viongozi zaidi wanaofanya kazi kwa weledi na ufanisi huku akiahidi kukitafutia fedha zaidi chuo hicho.

"Mzumbe ni Chuo chenye sifa ya kupika na kuzalisha viongozi mbalimbali wakiwamo wa Chama chetu cha Mapinduzi (CCM), kwa haraka Dk. Emmanuel Nchimbi na kwa upande wa serikali ni Balozi Ombeni Sifue ambaye bado tunamtumia kwenye shughuli za kiserikali," alisema.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema mahitaji ya sukari kwa sasa ni tani laki 650,000, upanuzi wa kiwanda hicho utaongeza uzalishaji hadi kufikia tani 271,000 kwa mwaka na idadi ya wakulima kutoka 9,500 mpaka 16,000 na mapato ya wakulima yatapanda kutoka Sh. bilioni 65 hadi bilioni 165.

Alisema wameanza kufanya upembuzi yakinifu wa kuwawekea wakulima wa miwa miundombinu ya umwagiliaji ili wafikie tija ya uzalishaji wa angalau tani 80 hadi 100, lengo likiwa ni asilimia 65 wa miwa ya kutumika katika uzalishaji sukari itoke kwa wazalishaji wadogo.

Msajili wa Hazina, Nehemia Msechu, alisema serikali inamiliki uwekezaji wa kiwanda hicho kwa asilimia 25 kupitia ofisi yake.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. Willium Mwegoha, alisema ujenzi wa majengo mapya chuoni umeshaanza na utagharimu Sh. bilioni 4.8 na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 15,000 hadi kufikia 40,000.

***Imeandaliwa na Jenifer Gilla na Ashton Balaigwa**

# Zitto alalama raia 162,000 kuzuiwa kukutana na wanasiasa, wizara yajibu

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe amelalama kuzuiwa kukutana na wananchi wapatao 162,000 walio katika kambi ya Kanonge na Katumba, wilayani Nsimbo, mkoani Katavi.

Amedai kuwa watu hao wamezuiwa kukutana na wanasiasa wa vyama vya upinzani nchini, akisisitiza ameshtushwa na hali hiyo kwa kuwa watu hao wana haki zote za uraia wa Tanzania.

Ameitaka serikali kumwagiza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuondoa wakuu wa makazi katika kambi hizo kwa madai kuwa wako kinyume cha sheria.

Zitto alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika Kata ya Ugalla jimboni Nsimbo.

Alisema viongozi wa ACT Wazalendo Mkoa wa Katavi waliandika barua kwa Jeshi la Polisi kutoa taarifa ya kufanya mikutano ya hadhara katika Kambi ya Kanonge, mkutano uliokuwa ufanyike juzi - Agosti 3 mwaka huu na kujibiwa kuwa Mkuu wa Makazi wa kambi hiyo ameeleza kuwa "siasa hairuhusiwi eneo hilo".

"Halmashauri ya Wilaya Nsimbo ilipokea zaidi ya wakimbizi 200,000 mwaka 1972 kutoka Burundi waliopelekwa katika kambi za Katumba na Kanonge, wilayani humo.

"Mwaka 2008 hadi 2010, serikali iliamua kutoa uraia kwa wakimbizi 162,000 waliokubaliwa kuwa raia wa Tanzania. Hawa wana haki zote zinazompasa raia wa Tanzania ikiwamo kuchagua na kuchaguliwa na ili haya yafanyike lazima wanasiasa tufike huko," Zitto alisema.

Aliongeza: "Wananchi wanaotambulika kuwa Watanzania kwa mujibu wa sheria za nchi katika kambi hizo, wanazo haki sawa na Watanzania wengine, hivyo kuzuia mikutano ya hadhara kufanyika eneo hilo ni kuwanyima haki yao kikatiba."

Zitto alisema kuwa mwaka 2020, walifanya mkutano katika Kambi ya Katumba kumwombea kura Philip Mallack kuwa Mbunge wa Nsimbo na wananchi hao walipiga kura, hali iliyomfanya ahoji mazingira ya kutoruhusiwa mikutano katika eneo hilo hivi sasa.

"Hizi ni mbinu za washindani wetu kuwatisha wakazi wa maeneo hayo. Mimi ninawaambia waacheni wawe na uhuru wa kuchagua wamtakaye, tusiwalazimishe kwa kuwa uraia wao si fadhila kwa chama fulani," Zitto alisema

Katika mkutano huo, Zitto pia alikosoa uamuzi wa serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuongeza maeneo ya hifadhi bila kujali ongezeko la idadi ya watu.

Alisema uamuzi huo ni sababu mojawapo ya kuongezeka migogoro kati ya wananchi na serikali katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Jimbo la Nsimbo.

Msemaji wa Chama cha ACT Wazalendo - Wizara ya Katiba na Sheria, Mbarala Maharagande, alihimiza wananchi wa kata hiyo kujitokeza kupiga kura na kugombea nafasi mbalimbali kwa tiketi ya chama hicho katika uchaguzi wa serikali za mitaa 2024.

"Mjitokeze ili mpate viongozi wazuri ambao watawajali na hawatawadai rushwa katika kutoa huduma mbalimbali," alisema Maharagande.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Christina Mwangosi, alipotafutwa na Nipashe kwa simu kuzungumzia suala hilo, aliahidi kutoa ufafanuzi ufafanuzi utatolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Wakimbizi.

Baada ya dakika chache, Mkurugenzi wa Idara ya Huduma kwa Wakimbizi, Sudi Mwakibasi, alisema kilichofanywa dhidi ya Zitto katika eneo hilo ni sawa kisheria kwa kuwa zuio la kufanya siasa katika maeneo wanamoishi wakimbizi ni la kisheria za ndani na kikanda zilizosimamiwa mkataba Umoja wa Afrika na wa Geneva wa Mwaka 1951, akidai zote zinakataza masuala ya siasa kufanyika ndani ya meneo hayo.

Alisema mkimbizi anapokuwa katika nchi iliyompa hifadhi, haruhusiwi kwa namna yoyote kushiriki baadhi ya shughuli za wazawa, ikiwamo siasa na mambo mengine ambayo yamo ndani ya katazo hilo.

Vilevile, mkurugenzi huyo alisema kuwa kwa mujibu wa sera ya nchi, wakimbizi wanapaswa kuhifadhiwa katika maeneo tengefu ambayo wataishi kwa kufuata sheria ikiwamo kutokushiriki kwa namna yoyote masuala ya kisiasa na uchaguzi.

Alisema pale ambapo kunatakiwa kufanyika kusanyiko lolote la zaidi ya watu watano katika maeneo hayo, wanatakiwa kuwa na kibali kutoka kwa mkuu wa makazi hayo.

"Kwahiyo, kilichofanyika kule (Zitto kuzuiwa), alichokifanya mkuu wa makazi ni kutekeleza sheria kwa sababu imekuwa ikizuiliwa kufanyika siasa na hata Watanzania waliomo ndani ya makazi wanapotakiwa kushiriki masuala ya uchaguzi, wanaandaliwa utaratibu nje ya makazi kwa sababu ni haki ya msingi," alisema.

## TANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

HABARI KITAIFA

SHERIA MPYA:

# Ukisifia 'cha Arusha' gereza linakuita

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana Dawa za Kulevya nchini (DCEA) iko katika mchakato wa kurekebisha sheria ili kudhibiti watu wanaosifia matumizi ya dawa za kulevya, ikiwamo bangi.

Imesema watu hao, wakiwamo wanamuziki wanaotumbuiza nyimbo au video zinazohamasisha matumizi ya dawa hizo, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Ofisa Sheria wa DCEA Kanda ya Kati, Meshack Lyabonga, alisema hayo juzi wakati wa semina iliyotolewa kwa viongozi wa dini, vyama vya siasa, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na waratibu wa uchaguzi mkoani Singida iliyoandaliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Alisema kumezuka tabia kwa baadhi watu, wakiwamo wasanii, kusifia matumizi ya dawa kulevya aina ya bangi, hali ambayo imekuwa ikihamasisha watu wengine kujiingiza katika matumizi yake.

"Maboresho haya ya sheria yakishakamilika, mtu akisifia dawa za kulevya, mfano akisema 'cha Arusha', 'cha Njombe kinafanya kazi hivi', akimaanisha bangi itakuwa ni kosa, na atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

Lyabonga alishauri Watanzania kuacha kusifia matumizi ya dawa za kulevya, ili taifa liwe na jamii iliyo safi na kwamba DCEA imeendelea kuongeza kasi kuwasaka na kuwakamata wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya wakiwamo 'mapapa' wa biashara hiyo haramu.

"Katika Kanda ya Kati ambayo DCEA inafanyia kazi katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Dodoma na Singida tunahakikisha dawa za kulevya hazipenyi. Tumefanikiwa kukamata dawa kadhaa katika mikoa hiyo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama," alisema.

Akizungumzia kilevi aina ya shisha, ofisa huyo alisema serikali itakuja na mwongozo wa matumizi ya shisha kwa kuwa limekuwa janga kubwa kutokana na watu wengi kukimbilia kutumia kilevi hicho ambacho kuna vitu vingi vinachanganywa ndani yake.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kukevya Duniani ya Mwaka 2023, takribani watu milioni 219 walitumia bangi mwaka 2021 sawa na asilimia nne ya watu duniani.

Pia inaonesha kwamba Afrika Kaskazini ni kitovu cha biashara ya bangi iliyosindikwa kupelekwa Ulaya Magharibi.

Matumizi ya bangi ni ya juu zaidi katika nchi za Afrika Magharibi na Kati na kufikia mwaka 2021 asilimia 10 ya watu (milioni 30) waliripotiwa kutumia bangi katika kipindi cha mwaka 2020, hususan katika nchi ya Nigeria.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa mazingira jiji la Arusha, Justin Rujomba (katikati) akielezea mipango ya kufikisha maji kwenye machimbo ya madini ya Tanzanite katika kikao cha eneo tengefu la Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, juzi, kulia ni Ofisa madini mkazi Mirerani, Nchagwa Marwa. **PICHA: GIFT THADEY**

# Benki CRDB yakabidhi gari kwa mwanafunzi wa udaktari

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KWA mara ya kwanza mwanafunzi wa udaktari katika Chuo Kikuu cha Tiba cha KCMC, Hussein Hamadi amekuwa mshindi wa gari aina ya Nissan Dualis.

Hussein amekabidhiwa gari hilo ambalo ni la pili kutolewa mwaka huu katika viunga vya Chuo Kikuu cha Tiba KCMC mwishoni mwa wiki mbele ya wanafunzi wenzake, walimu na wafanyakazi wa chuo hicho.

"Ninajisikia furaha sana kushinda gari hili," alisema Hamadi baada ya kukabidhiwa kadi ya gari, ufunguo pamoja na nyaraka za bima kubwa.

Ushindi wa mwanafunzi huyo wa fani ya fiziotherapia ulitangazwa na Meneja wa Huduma za Benki CRDB kupitia Simu, Emmanuel Moshi katika droo ya pili ya mshindi wa gari iliyofanyika mwezi uliopita.

"Ilikuwa ni bahati yake kwa kweli kwani kabla yake, walipigiwa simu wateja wawili. Mmoja hakupatikana kabisa ila mwingine simu yake iliita lakini hakupokea.

"Utaratibu unatutaka kumpigia mteja mara tatu na kama hatopatikana au hatopokea basi droo inarudiwa, ndivyo kwa Hussein," alikumbusha Moshi jinsi mchakato huo ulivyokuwa.

Hussein alikabidhiwa gari hilo na Meneja Biashara wa Kanda ya Kaskazini wa Benki ya CRDB, David Peter aliyesema matumizi ya huduma za Simbanking yanazidi kuongezeka na benki inaendelea kuhamasisha wateja wake kuzitumia ili kuingia katika uchumi wa kidijiti ambao ndio mwelekeo wa dunia kwa sasa.

Mshauri wa Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tiba cha KCMC, Anza Lema alisema ushindi wa Hussein umeleta furaha kwa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wa chuo hicho ambao nao wamehamasika zaidi kutumia huduma za Simbanking.

"Wengi hatukuwa tunaamini kuwa unaweza kushinda lakini Hussein ametuthibitishia kuwa ni suala linalowezekana, hamasa imeongezeka miongoni mwetu," alisema Lema.

Naye Peter alisema, "Kampeni yetu ya 'Benki ni Simbanking' ni ya mwaka mzima. Kila mwezi huwa tunawatangaza washindi wawili wa bodaboda na mmoja wa bajaji.

"Mshindi wa gari tunampata kila baada ya miezi mitatu. Aprili tulimpata mshindi wetu wa kwanza wa Nissan Dualis na Julai tumempata Hussein. Ninawakaribisha wateja wetu wote na Watanzania kwa ujumla kuendelea kutumia huduma za Simbanking ili nao wawe sehemu ya ushindi huu," alisema Peter.

Tangu zawadi zilipoanza kutolewa, Peter alisema tayari pikipiki nane, bajaji tatu pamoja na magari mawili sasa yameshatolewa. Mbali na vyombo hivyo vya usafiri, Peter alisema zawadi nyingine zinazotolewa ni kompyuta mpakato kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, fedha taslimu, pointi za tembo zinazoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu, simu za mkononi, chupa za maji na nyinginezo. "Lengo la kampeni hii ni kumpunguzia mteja gharama ili afanye kila muamala anaotaka akiwa mahali alipo kupitia huduma zetu za Simbanking. Huduma hiii imedumu sokoni kwa zaidi ya miaka 15 sasa, ni njia rahisi ya kupata huduma za Benki ya CRDB," alisema Peter.

Alisema huduma za Simbanking zinatolewa kwa kutumia teknolojia ya hali ya juu ambayo ni salama na ya uhakika, inayowezesha wateja kupata huduma kupitia simu za mkononi.

Hivi sasa, wateja wa Benki ya CRDB wanaweza kupata zaidi ya asilimia 95 ya huduma kidijiti wakiwa mahali popote.

Ili kushinda moja ya zawadi zinazotolewa na Benki ya CRDB, alisema mteja anatakiwa kufanya miamala mingi kupitia Simbanking kama vile kulipia bili za umeme na maji, kukata tiketi ya usafiri wa ndege, kulipa ada na michango ya shule, kulipia bidhaa zinazouzwa mtandaoni au kununua muda wa maongezi na huduma nyingine nyingi zinazopatikana ndani ya Programu ya Simbanking.

"Sifa zilizowapa ushindi wateja hawa watatu zinawezekana kwa mteja mwingine yeyote wa Benki ya CRDB, hivyo niwahimize wateja wetu wote kutoka mahali popote walipo kuendelea kutumia huduma za Simbanking ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kushinda zawadi kemkem tulizonazo," alisema Peter.

# Spika Tulia ahadharisha matumizi Akili Mnemba

**Na Maulid Mmbaga**

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson amesema ni muhimu kuwa makini katika matumizi ya akili mnemba (AI) na athari zake zizingatiwe kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

AI ni nadharia na uundaji mifumo ya kompyuta yenye uwezo wa kutekeleza kazi ambazo kwa kawaida zinahitaji akili ya binadamu kama kuona, kutambua sauti, kufanya uamuzi au kutafsiri lugha. Inatumika zaidi viwandani, serikalini na kwenye utafiti wa kisayansi.

Spika Tulia aliyekuwa akizungumza wakati wa kongamano la kukusanya maoni kuhusu Dira Mpya ya Maendeleo ya Taifa 2050 jijini Mbeya juzi, alisema ni muhimu kupanga mipango ya nchi kwa kuzingatia mikakati na mapinduzi yanayotokea kila siku kote duniani.

"Nikiwa kama Rais wa Mabunge Duniani (IPU), ninatembelea nchi mbalimbali na kujionea hatua mbalimbali za kimaendeleo zinazopigwa kwenye nyanja ya sayansi na teknolojia, maendeleo yake yanaibadilisha dunia kwa kasi na hivyo kuwa na uwezo wa kuathiri mifumo yetu ya kimaisha, mambo haya lazima yatutafakarishe," alisema Dk. Tulia.

Pia alisisitiza umuhimu wa ulinzi wa demokrasia na haki za binadamu, akisema maendeleo ya teknolojia yameweka shakani masuala hayo kutokana na matumizi ya AI na vifaa vingine vya kiteknolojia ambavyo vikitumika vibaya vinaweza kuharibu demokrasia na kufifisha haki za kibinadamu.

Katika hatua nyingine, Spika Tulia amesema magonjwa ya mlipuko, gharama za vyakula, viwango vya juu vya riba za mikopo, mabadiliko ya tabianchi, hatari mbalimbali za kijiografia pamoja na uhaba wa nishati safi na salama, ni vihatarishi vya kuzingatia katika kuandaa dira hiyo.

"Ni matumaini yangu kuwa uandishi wa dira kupitia maoni ya wananchi na timu ya wataalamu utazingatia changamoto hizi za kidunia na kuzitolea mapendekezo ya kimkakati katika utekelezaji wake," alisema Dk. Tulia.

Alitaja maeneo ya kutiliwa mkazo kwa vijana katika dira hiyo, ikiwamo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), burudani na sanaa, shughuli zinazochipukia pamoja na kilimo cha kisasa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mashabiki Yanga wazoeshwe utamaduni wa kununua tiketi

**SOKA** ndio mchezo pendwa zaidi duniani na unawaingizia wachezaji na klabu kipato kikubwa sana, hivyo kuwa biashara inayoingiza mabilioni ya pesa kwa muda mfupi zaidi.

Kwa hapa Tanzania tu, zinaweza kutengenezwa mpaka Sh. milioni 500 mpaka 700 kwa dakika 90 tu kwa viingilio vya uwanjani kwa zile mechi kubwa na zenye mvuto.

Viingilio hivi vinatokana na pesa za mashabiki ambao wanakata tiketi kwa ajili ya kushuhudia mchezo husika.

Huko Ulaya na mabara mengine imeshuhudiwa kiasi kikubwa zaidi cha mabilioni kikipatikana kwani tiketi zake huuzwa ghali sana, na wakati mwingine kuna mashabiki hununua hata tiketi za msimu nzima.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), hapa nchini Simba ndiyo timu inayoongoza kwa kuingiza pesa nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, achilia mbali kwenye mechi za kimataifa ambazo mara nyingi huujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa. Hii ina maana mashabiki wake wanaingia uwanjani kwa kulipa wenyewe viingilio, hata kama ni kikubwa, ili mradi tu akaione na kuishangilia timu yake.

Simba imekuwa ni timu ya mfano si hapa Tanzania tu, bali hata Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), limewataja mashabiki wake kuwa ni mfano wa kuigwa pale linapokuja suala la mechi za kimataifa ambapo msimu uliopita liliwazawadia tuzo ya Mashabiki Bora kwenye michuano ya African Football League, AFL.

Mashabiki wa Simba wanaweza wasijae katika mechi za Ligi Kuu, lakini linapokuja suala la mechi za kimataifa ni habari nyingine, ndiyo maana CAF ilitoa tuzo hiyo msimu uliopita.

Sababu ni moja tu, hukata tiketi na kuingia bila kupewa ofa ya kuingia bure. Kwa Yanga hili jambo bado lina uzito, kwani mashabiki wake wameendelea kuwa na kasumba ya kutaka tiketi za bure ili waende mpirani.

Na tatizo siyo wao, bali viongozi ndiyo wanalilea hili kiasi kwamba tumeona hata Wiki ya Mwananchi wapo walioingia kutokana na tiketi za bure walizozawadiwa baada ya kuchangia damu, tofauti na wenzao Simba ambao walijaza siku tatu kabla ya Tamasha la Kilele cha Simba Day.

Sijawahi kusikia viongozi wa Simba wakigawa tiketi bure, lakini mara kwa mara tumekuwa tukishuhudia baadhi ya viongozi wa Yanga wakinunua tiketi na kuzigawa.

Hii si nzuri hata kidogo kwa afya ya soka kwa sababu ikija siku sasa wanahitajika mashabiki waingie kwa tiketi zao inakuwa ngumu kwani wengi hutegea wakisubiri itangazwe ofa ya kuingia bure.

Tunatambua klabu nyingi duniani hujiendesha kwa pesa za wadhamini, jezi, mapato ya milangoni na vitu vingine vinavyofanana na hivyo. Kwa sasa Kampuni ya GSM ndiyo inafanya kazi kubwa ya kuifanya Yanga iwe hapo, cha kujiuliza kama siku ikiamua kuondoa nini kitatokea kama mashabiki wanataka tiketi za bure. Je, ikija sheria ya klabu kutumia mapato yake kujiendesha Yanga itaweza kufanya hivyo kweli?


Sisi tunaona ni wakati sasa kwa viongozi wa Yanga kuachana na woga au mashindano yasiyo na tija ya kuonekana kuzidiwa na Simba, badala yake kuwaacha mashabiki wanunue wenyewe hata kama watakaoingia uwanjani kwa kununua tiketi watakuwa robo, lakini baada ya muda watajua wajibu wao.

Kwa upande wa mashabiki nao, hawawatendei haki viongozi wao wanaofanya kila kitu kwa ajili yao, lakini kununua tiketi inakuwa shida.

Inakuwaje timu ina Pacome Zouzoa, Stephane Aziz Ki, Maxi Nzengeli, Clatous Chama, Prince Dube na nyota wengine kibao, lakini bado shabiki ununuliwe na kupewa tiketi ya bure kwenda uwanjani? Huu ni wakati wa kubadilika sasa na kuipa thamani klabu yenu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wenye tenda za jezi wajue pia kuna mashabiki wanene

Na Adam Fungamwango

**WAKATI** klabu kongwe za Simba na Yanga zikitoa jezi za msimu kumekuwa na malalamiko kuwapo kwa uhaba au kutokuwapo kabisa za watu wenye miili mikubwa, maarufu mabonge.

Malalamiko kutoka sehemu mbalimbali kwa watu hao, wanasema wamekuwa wakihaha kutoka duka moja mpaka lingine kwa ajili ya kusaka jezi saizi zao na imekuwa ni aghalabu sana kuzipata.

Uchunguzi mdogo nilioufanya kwa watu waliokuwa wanalalamika, inaonyesha kuwa jezi mpya za Yanga msimu huu ndizo zinazolalamikiwa sana kuwa nyingi saizi zake ni ndogo na mashabiki wamekuwa wakipata shida kuzipata.

"Mimi nimetembea maduka zaidi ya matano kutafuta saizi yangu sijaipata na siyo mimi tu, nikawapigia mashabiki wenzangu wa Yanga ambao ni vibonge kama mimi, wakaniambia hata wao wanahangaika kuzitafuta, hii inatukatisha tamaa, inakuwaje walete saizi moja, au watusahau watu kama sisi," alilalamika mmoja wa mashabiki ambaye hakutaka jina lake liwekwe hadharani.

Malalamiko ya mashabiki hao na wengine ambao mpaka sasa wengine kwa wiki nzima bado wanazisaka ni kuwasilisha kilio chao kwa wenye zabuni na waagiza jezi kutambua kuwa binadamu hawafanani.

Kuna warefu, wafupi, wembamba, wastani na wanene zaidi. Hawa wote wana mahitaji sawa, ikiwamo nguo, viatu, kofia na mambo mengine.

Ndiyo maana tunaona kuna nguo zenye saizi tofauti kuanzia za kiume mpaka za kike, kuna nyembamba ambazo watoto wa mjini wanaziita 'modo', mpaka zile pana ambazo zinavaliwa na watu wenye miili mikubwa.

Hata viatu kuna saizi kuanzia za watoto mpaka kwa wale wenye miguu mikubwa mno, nao pia wanapata viatu vyao, iweje isiwe jezi?

> **Malalamiko ya mashabiki hao na wengine ambao mpaka sasa wengine kwa wiki nzima bado wanazisaka ni kuwasilisha kilio chao kwa wenye zabuni na waagiza jezi kutambua kuwa binadamu hawafanani.**

"Jamani mbona jezi za watoto zinatengenezwa kwa wingi, halafu siku hizi kuna mpaka jezi za wanawake ambazo zinatengenezwa kwa mtindo tofauti na jezi za kawaida, inakuwaje wasitengeneze saizi kubwa nyingi?" Akauliza mteja mwingine katika duka mmoja Sinza jijini Dar es Salaam.

Inawezekana ikawa zinatengenezwa, lakini nadhani makadirio ya waagizaji ndiyo yanayokuwa si sahihi.

Inaonekana wanakadiria kuwa watu wenye miili mikubwa ni wachache sana nchini kuliko wenye miili ya kawaida.

Najua hawapo mbali na ukweli, lakini dunia ya sasa tuliopo hasa hapa nchini na kutokana na mtindo wa maisha, kumekuwa na ongezeko la watu wenye miili mikubwa.

Hata wale ambao zamani walikuwa na miili midogo wameshaanza kuwa na vitambi, pamoja na kunenepa, hivyo nadhani hata watengeneza na waagiza jezi wanatakiwa watambue hilo na mzigo wa jezi za watu wanene uongezwe.

Halafu cha kufurahisha zaidi ni kwamba wengi wenye miili hiyo ndiyo wenye pesa, hivyo kutokuwapo kwa jezi za aina hiyo pia inazikosesha klabu na hata wao wenyewe wafanyabiashara na nchi kwa ujumla kukosa kodi.

Nadhani baada ya malamiko yao, na mimi kuyawasilisha hapa kuna kitu mtakuwa mmejifunza, mzigo utakaokwenda kutengenezwa au kuagizwa tena, basi oda za watu wanene ziongezwe kwani na wao wanataka kuvaa jezi kufurahia timu zao kama wengine.

# Wizi wa mafuta watikisa ujenzi wa barabara

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara amesema wako katika msako wa kubaini watu wanajiohusisha na wizi wa mafuta katika ujenzi wa barabara kutoka Wilaya ya Newala - Masasi Km 60 zinazojengwa kwa kiwango cha lami.

Louter Kanoni aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wakuu wa idara, vitengo, watendaji wa kata na madiwani katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Katika kikao hicho, Kanoni alisema kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya imeshaanza ufuatiliaji wa wizi huo wa mafuta Ili kuwabaini wale wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Alisema kuwa katika eneo la Kata ya Chiungutwa ndiko kuna kituo cha kampuni inayotekeleza ujenzi wa barabara hiyo.

Alisema kuwa kituoni huko kumekithiri wizi wa mafuta aina ya dizeli unaofanywa na watu wasiojulikana.

Kanoni alisema vitendo hivyo ni ishara ya kuwapo hujuma katika mradi huo zinazoweza kuathiri utekelezaji wa mradi huo.

"Baada ya kupata taarifa hizi za kukithiri wizi wa mafuta katika mradi huu wa barabara, tumesikitika sana na tayari kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya inaendelea kufanya ufuatiliaji ili kubaini wale wote wanajiohusisha na vitendo hivi," alionya Kanoni.

Mkuu wa Wilaya aliyataja maeneo ambayo ndio yamebainika wezi hao wa mafuta wanatoka na kujihusisha na vitendo hivyo vya wizi wa mafuta ya mradi huo wa barabara kuwa ni vijiji vya Mitesa, Msanga, Mitesa na Nagaga.

Alisema kuwa kwa sasa wilayani Masasi kumekuwa na wahamiaji ambao wamekuwa wanatoka katika maeneo mbalimbali wa wilaya za jirani, baadhi yao wanajihusisha na wizi huo wa mafuta.

Alisema ufuatiliaji wa awali unaonesha wezi wa mafuta hayo wengi wao si wenyeji wa maeneo hayo, bali wageni waliofika katika vijiji hivyo na kufanya wizi huo.

Kanoni alisema watu hao ni wazoefu wa kuiba mafuta kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo huko walikotoka.

Alisema kuwa kwenye maeneo ya Wilaya ya Masasi wamekuwa wanapanga katika nyumba za wenyeji na kufanikisha wizi huo.

"Niombe watendaji wa kata, waheshimiwa madiwani, watendaji wa vijiji, nendeni mkawatambue watu ambao wako huko wamekuja kwa shughuli zipi?

"Kama kuna wenyeji, basi tuwatahadharishe, hii si dalili nzuri... na sisi kupitia vyombo vyetu vya dola tutaendelea kufanya ufuatiliaji tutawakamata," aliagiza.

Akizungumzia mradi huo wa ujenzi wa barabara, kiongozi huyo alisema kuwa kuwa hivi sasa tayari vifaa vingi vya ujenzi wa barabara hiyo, ikiwamo mitambo na magari, vimeletwa.



Naibu Spika Mussa Zungu (wa pili kushoto) akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bank of Africa, Esther Cecil Maruma (katikati) wakati wa hafla ya siku ya uhuru wa Morocco mwishoni mwa wiki. Wengine ni Balozi wa Morocco nchini, Zakaria El Goumiri (wa pili kulia) na Manaibu Wakurugenzi wa Bank of Africa,Wasia Mushi (kushoto) na Hamza Cherkaoui. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge atimuliwa Baraza la Madiwani

## -DC aingilia kati, madiwani wapiga kura

**Na Vitus Audax**, MBOGWE

BARAZA la Madiwani wilayani Mbogwe, mkoani Geita limemfukuza katika kikao chake, Mbunge wa Jimbo hilo, Nicodemus Maganga baada ya kushinikiza kuondolewa vizuizi vya ukusanyaji ushuru wa mazao kwa wakulima vinavyolalamikiwa kutumika kunyanyasa wakulima.

Awali akizungumza katika kikao hicho juzi, Mbunge Maganga alisema vizuizi hivyo vimekuwa kero kwa wakulima kutokana na kutumika kuwatoza ushuru mkubwa pasi na kupatiwa risiti.

"Miongoni mwa kero kwa wakulima ni haya mageti mliyoyaweka tarehe 16 mwezi wa nne (Aprili) yameleta malalamiko sana kwa wananchi. Ninaomba basi unipe nafasi mwenyekikti au ueleze wewe mwenyewe," alisema Maganga katika kikao hicho.

Ni hoja iliyopingwa vikali na baadhi ya madiwani katika baraza hilo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Vicent Busiga akatoa amri mbunge huyo aondoke katika kikao hicho na sehemu ya majibizano yao ikawa hivi:

Mwenyekiti: Sasa kama mwenyekiti wa kikao ninasiamia kanuni, ninaomba utoke nje.

Mbunge" Sasa hivi? Hamna sitoki!

Mwenyekiti: Nitatumia utaratibu utoke.

Mbunge; Hamna sitoki na hapa sasa utajua mimi ni nani na hapa ninazungumia ukurasa wa 111, sawa? Kwa maana hiyo Mwenyekiti... (akakatishwa).

Mwenyekiti: Sijakuruhusu.

Kutokana na majibizano hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Sakina Mohamed aliingilia kati na kueleza sababu zilizoilazimu halmashauri hiyo kuweka vizuizi hivyo vya kukusanya ushuru.

Hata hivyo, maelezo hayo ya Mkuu wa Wilaya yakaibua mvutano zaidi katika kikao hicho cha Baraza la Madiwani.

"Tukumbuke pia kwanini mwananchi anaanza kukuuliza kuhusu hili, inapofika muda huu mnaongeza mageti ya vizuizi hivi, mnaelewa madhara yake yalivyo makubwa? Inawezekana hapa kuna watu mnatengenezeana ajali za chama kushindwa baadaye," Sakina alisema.

Kutokana na mvutano huo, Mwenyekihti wa Baraza hilo, Busiga, aliitisha kura ya maoni kwa madiwani wanaopinga na wanaokubali kuwapo vizuizi hivyo ili kuondoa vurugu katika kikao hicho.

"Hoja ikileta mvutano, mimi ninasimama kwenye kanuni na hapa ninaomba kutangaza kuwa walioshinda mageti yawapo ni watu 19, hivyo hao ndio wameshinda, ninaomba mageti yaendelee kuwapo," Mwenyekiti Busoga alifunga hoja hiyo huku Mbunge Maganga naye akiendelea kuwa sehemu ya madiwani hao katika kikao hicho.

**KABWELA** — **Na Fadhili Mohammed**







# 'Msigawe vitambulisho vya NIDA kama pipi'

**Na Vitus Audax,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo ameagiza Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuhakikisha inazingatia vigezo vilivyowekwa kisheria katika usajili na utoaji vitambulisho vya taifa ili kuepuka kuwapa watu wasiokuwa raia wa Tanzania.

Alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki jijini Mwanza wakati akizungumza na watumishi wa vyombo vya usalama vilivyopo chini ya wizara hiyo; Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Uangalizi pamoja na NIDA. "Msigawe vitambulisho vya taifa kama pipi, zingatieni vigezo vilivyowekwa kisheria, hivi ni usalama wa nchi yetu, hakikisheni mnazingatia vigezo kwa wale wanaostahili vitambulisho hivyo wanavipata kwa ajili ya matumizi mbalimbali," aliagiza Sillo.

Naibu Waziri huyo alisema kuwa hadi kufikia Agosti mwaka huu, Watanzania zaidi ya milioni 24 wamesajiliwa katika mfumo wa NIDA huku zaidi vitambulisho milioni 21 vimezalishwa kupitia mamlaka hiyo na kati ya hivyo, vitambulisho milioni 20 vimesambazwa kwa wananchi. Kuhusu usambazaji vitambulisho hivyo, Naibu Waziri Sillo aliagiza mamlaka hiyo kuhakikisha inashusha kadi zote ambazo zimekamilika hadi ngazi za vijiji ili wananchi wazipate kwa urahisi.

"Kwa zile kadi ambazo zipo kwenye maeneo yetu, shusheni chini kwenye kata na vijiji ili wananchi wapate vitambulisho vyao vya taifa ambavyo vimekamilika kwa ajili ya matumizi kwenye huduma mbalimbali zinazotolewa nchini," aliagiza Naibu Waziri Sillo.

Katika ziara yake ya siku mbili mkoani Mwanza, Naibu Waziri Sillo alifanya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa vituo vya polisi vinavyojengwa kwa nguvu za wananchi ikiwa ni pamoja na Kituo cha Polisi Nyegezi, wilayani Nyamagana, Kituo cha Polisi Nyamohongolo kilichoko Ilemela na Zahanati ya Polisi Mabatini.

Akizungumza baada ya kikao hicho, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna Msaidizi wa Polisi (DCP), Wilbrod Mutafungwa, alihakikishia wizara kuwa wataendelea kusimamamia nidhamu, hasa kutojihusisha kabisa na vitendo vya rushwa.



Msajili laini wa Airtel Tanzania, Mariam Marco akitoa huduma kwa mmoja ya wateja kwenye Banda la Airtel Tanzania katika Maonesho ya Nanenane eneo la Nyamhongolo, mkoani Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumo dume watajwa kikwazo kwa wanawake kuwania nafasi za uongozi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya wanawake wanaoishi katika maeneo ya vijijini wamesema mila na desturi kandamizi, ukiwamo mfumo dume, limeendelea kuwa kikwazo kwa baadhi yao na kufanya washindwe kushiriki kuwania nyadhifa mbalimbali za uongozi serikalini.

Walibainisha hayo juzi kwenye mdahalo ulioandaliwa na Shirika la WEADO katika Kata ya Lyabukande, wilayani Shinyanga, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji Mradi wa Chukua Hatua Sasa Zuia Ukatili kwa ufadhili wa Mfuko wa Ruzuku za Wanawake (WFT-Trust).

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake katika Kata hiyo, Mary Revocutus, alisema wanawake wengi wanakabiliwa na vikwazo vinavyotokana na mfumo dume, ambao huwafanya waogope kugombea nafasi za uongozi kwa kuhofia kupigwa na waume zao na hata kuvunja mji.

"Huku mwanamume ndiye mwenye sauti na uamuzi wa kila kitu. Ikiwa mume wako hajaunga mkono azma yako ya kugombea, huwezi hata kuchukua fomu," alisema Mary.

Diwani wa Viti Maalum Kata ya Layabukande, Eunice Magese, aliomba wanaume kuacha kuendekeza mila kandamizi pamoja na wivu kwa wake zao, bali wawape rukhusa wagombee nafasi za uongozi na kukiri tatizo hilo kuwa kubwa katika maeneo hayo.

Alisema kuwa katika safari yake ya kisiasa, mume wake alikuwa naye bega kwa bega na hata kumpatia fedha za kuendesha kampeni hadi kufanikiwa kupata nafasi ya udiwani wa viti maalumu.

Diwani Zawadi Mwasha alishauri kutoa elimu kwa wanaume kuhusu umuhimu wa kuachana na tamaduni za zamani na kuimarisha usawa wa kijinsia sambamba na kudhibiti rushwa ya ngono.

Mzee maarufu katika kata hiyo, Peter Amosi, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo la mila kandamizi, akiongeza kuwa wanawake wa vijijini mara nyingi wanaonekana kuwa chini ya wanaume, na hivyo ni vigumu kwao kuwa viongozi.

Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji kutoka Shirika la WEADO, John Eddy, alisema wameendesha mdahalo huo kwa lengo la kuhamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani pamoja na kushiriki kupiga kura ili kufikia usawa wa kijinsia katika nafasi za uongozi.

# Wananchi wajenga zahanati

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kijiji cha Idetemya, Kata ya Bulungwa, Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga, wamelazimika kuchangishana Sh. 10,000 kila kaya na kuanzisha ujenzi wa zahanati ya kijiji.

Lengo la ujenzi huo ni kukabiliana na vifo vya wajawazito vitokanavyo na uzazi; wajawazito katika kijiji hicho wakiripotiwa kujifungulia njiani wakati wanakwenda zahanati jirani kupata huduma.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Daudi Masanja alisema tayari ujenzi wa msingi wa zahanati hiyo umeanza, ukijumuisha vyumba 15 na kuwa hatua hiyo itasaidia kuondokana na adha ya kutembelea umbali mrefu kufuata huduma.

Masanja alisema kuwa kupitia michango hiyo, wamekusanya Sh. milioni 2.28. Kati yake, Sh. milioni 2.145 zilitumika kuanzisha ujenzi wa msingi wa zahanati na kulipa gharama za mafundi, hivyo kumwomba mbunge kuwachangia kufanikisha ujenzi huo.

Akieleza adha wanazokutana nazo wanawake wakati wa kujifungua, mkazi wa kijiji hicho, Sauda Juma alisema baadhi yao wamekuwa wakijifungulia njiani wakati wakienda vijiji jirani kutafuta huduma za uzazi.

Alisema kutoka kijijini huko hadi Mseki iliko zahanati jirani ni kilometa 12, kwenda Idahina-Mpunze kilometa 10 na Bunada-Nyankende ni kilometa nne mpaka tano na wengi wanatumia usafiri wa baiskeli.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Charahani aliingiwa na hofu ya kutokuwapo matumizi sahihi ya fedha zilizotolewa na wananchi.

Alisema kuwa mbali na kutolewa Sh. 10,000 kwa kila kaya, vifaa mbalimbali vya ujenzi, yakiwamo mawe na mchanga, hakukuwa na haja kutumia Sh. milioni 2.145 kati ya Sh. milioni 2.28 kujenga msingi.

"Kamati mnapokwenda kukubaliana na mafundi katika kuanzisha ujenzi wa umma, kubalianeni bei nzuri kama mnajenga makazi yenu na si kuongeza cha juu ili kujinufaisha wenyewe.

"Hamwezi kujenga msingi wa zahanati kwa Sh. milioni 2.145 na huku eneo la ujenzi kulikuwa na vifaa vya ujenzi ambavyo pia vilitolewa na wananchi," alisema Charahani. Alitaka kamati ya ujenzi kupiga upya hesabu zao na kuangalia wapi wameteleza ili kurejesha fedha zinazodaiwa kuibwa zaidi ya Sh. 700,000 ili kutowavunja nguvu wananchi kujitoa kujiletea maendeleo kwa kusogeza huduma za afya karibu na makazi yao.

Ibara ya 8(1d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inaelekeza wananchi kushiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya katiba hiyo.

Nipashe
Spotika




HUYU NDIYE CALAFIORI WA ARSENAL UK. 12-13




# WACHEZAJI 10 WALIOPANDA THAMANI ZA UHAMISHO 2024

## ISIKUPITE

NI miaka 60 imepita tangu mwanamichezo wa mazoezi ya viungo (artistic gymnast) kutoka Soviet, Larisa Latynina, alipoweka rekodi kwenye Olimpiki ya Tokyo 1964 kwa kuwa mwanamichezo mwenye medali nyingi zaidi duniani, lakini sasa ukurasa mpya umefunguliwa baada ya mwanadada Mmarekani, Katie Ledecky, Jumamsi iliyopita kwenye Paris 2024 kuifikia kwa kutwaa medali ya tisa kwenye mchezo wa kuogelea mita 800 freestyle.



**LONDON,** England

MWAKA 2024 umeshuhudia idadi ya wachezaji wachanga wanaonekana kutoka nje na baadhi kuwa wanasoka bora zaidi duniani.

Na, kama unavyotarajia madili ya uhamisho wa wachezaji yamepanda kwa matokeo.

Hawa ndio wachezaji 10 ambao thamani zao za uhamisho zimeongezeka zaidi mwaka wa 2024.

Ingawa msimu wa 2023/24 ulikuwa janga kamili kwa Bayern Munich, kuibuka kwa Aleksandar Pavlovic kulikuwa angalau chanya. Kiungo huyo alikua mchezaji muhimu kwa 'Bavaria' hao msimu wa 2023/24, na kucheza mechi 19 za Bundesliga.

**9. Pau Cubarsi**
**Thamani ya sasa: Euro milioni 30**
**Ongezeko: Euro milioni 28.5**

Mikono juu ikiwa unajua Pau Cubarsi alikuwa nani kabla ya 2024? Isipokuwa wewe ni mshabiki makini wa Barcelona B, kuna uwezekano kwamba unadanganya kwa kuinua mkono wako juu.

Kama ushahidi wa ongezeko kubwa la thamani yake ya uhamisho, beki huyo alitoka kwenye hali ya kutofahamika mwaka 2024 na kuwa mmoja wa majina ya kwanza kwenye jedwali la timu ya Barca na mchezaji wa kimataifa wa ngazi ya juu wa Hispania. Amefanya yote haya akiwa na umri wa miaka 17. Hiyo ni nzuri sana kwake.

**8. Arda Guler**
**Thamani ya sasa: Euro milioni 45**
**Ongezeko: Euro milioni 30**

Baada ya kujitahidi sana kupata utimamu wa mwili mwaka 2023 na muda wa mchezo kwa sehemu kubwa ya 2024, kipindi cha miezi mitatu kati ya Mei na Julai kilithibitika kuwa kizuri sana kwa thamani ya uhamisho ya Guler.

Kiungo huyo mshambuliaji alikuwa na kiwango bora katika ngazi ya klabu na kimataifa, akifunga mabao manne katika mechi tatu za mwishoni mwa msimu wa La Liga akiwa na Madrid na alifunga mabao matatu akiwa na Uturuki iliyotinga robo fainali ya Euro 2024.

**7. Florian Wirtz**
**Thamani ya sasa: Euro milioni 130**
**Ongezeko: Euro milioni 30**

Ikiwa kuna njia moja ya kufupisha jinsi Florian Wirtz alivyokuwa mzuri mnamo 2023/24 ni hii: Aliipa Bayer Leverkusen taji lao la kwanza kabisa la Bundesliga.

Hilo ni jambo ambalo Michael Ballack hakuweza kufanya. Hilo ni jambo ambalo Dimitar Berbatov hakuweza kufanya. Hilo ni jambo ambalo Toni Kroos hakuweza kufanya.

Euro milioni 130 ni hesabu ya haki ya mchezaji kama huyo kwenye vitabu.

**6. Vinicius Junior**
**Thamani ya sasa: Euro milioni 180**
**Ongezeko: Euro milioni 30**

Mchezaji wa thamani zaidi kwenye orodha hii ni Vinicius Junior.

Supastaa huyo wa Brazil alitamba sana msimu wa 2023/24, akifunga mabao kadhaa muhimu katika harakati za kufanikiwa za Real Madrid kushinda taji la LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya - hata alifunga katika fainali.

Ndiye mchezaji anayepewa nafasi zaidi ya kutwaa Ballon d'Or.

**5. Riccardo Calafiori**
**Thamani ya sasa: Euro milioni 45**
**Ongezeko: Euro milioni 32**

Kulingana na Transfermarkt, Arsenal walitumia zaidi ya euro milioni nne kwa Riccardo Calafiori.

Wamejinyakulia mchezaji mzuri, kwani beki huyo ndiye aliyeibuka kidedea msimu huu kwenye Serie A, na alivutia sana kwenye euro 2024.

**4. Cole Palmer**
**Thamani ya sasa: Euro milioni 80**
**Ongezeko: Euro milioni 35**

Katika miezi 12 iliyopita, Cole Palmer ametoka kupasha moto benchi Manchester City hadi kushinda Mchezaji Bora Chipukizi wa Mwaka na kufunga bao kwenye fainali ya Euro 2024.

Kwa hiiyo kama inavyotarajiwa thamani yake ya uhamisho imepanda sana.

**3. Phil Foden**
**Thamani ya sasa: Euro milioni150**
**Ongezeko: Euro milioni 40**

Ajabu, thamani ya awali ya Phil Foden ya uhamisho ilikuwa isiyo na kikomo na kwa kweli ameweza kupanda kutokana na kampeni bora akiwa na Manchester City.

Kiungo huyo mshambuliaji alikuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu msimu uliopita, akifunga mabao 27 katika mechi 35 alizocheza.

**2. Kobbie Mainoo**
**Thamani ya sasa: Euro milioni 55**
**Ongezeko: Euro milioni 49**

Ongezeko la euro milioni 49 utashangaa zaidi. Kobbie Mainoo mwaka 2024 alikuwa mchezaji mchanga mwenye kusisimua zaidi katika Ligi Kuu England na mchezaji wa kawaida wa England - akianza mechi zote za raundi ya mtoano ya taifa lake kwenye Euro 2024.

**1. Lamine Yamal**
**Thamani ya sasa: Euro milioni 120**
**Ongezeko: Euro milioni 60**

Bila shaka Lamine Yamal yuko juu ya orodha. Pasi na shaka alikuwa mchezaji bora zaidi katika Euro 2024, yeye ndiye mchezaji mchanga anayevutia zaidi katika soka kidunia, na mchezaji bora zaidi kutoka La Masia tangu Lionel Messi.

## Extra Time

# HUYU NDIYE CALAFIORI WA ARSENAL



CALAFIORI

**LONDON,** England

WAKATI Klabu ya Bologna ilipotangaza kuwasili kwa Riccardo Calafiori kutoka FC Basel mwishoni mwa Agosti mwaka jana, saa chache tu kabla ya kumalizika kwa dirisha la uhamiaji la wachezaji, wachache sana walikisia jinsi hatua hiyo ingefanikiwa.

**Kutokana na kuwasili kwa Jose Mourinho huko AS Roma mwaka 2021, jiji la nyumbani la Calafiori na klabu aliyokulia, nafasi na wakati wa kucheza vilikuwa adimu kwa beki huyo.**

Hilo lilimtia moyo kukubali uhamisho wa kudumu kwenda kwa wababe wa Uswisi, Basel katika msimu wa 2022.

Licha ya kuwa mara kwa mara katika timu za vijana za Italia, Calafiori alianza kuteleza kutoka kwenye rada ya soka la Ulaya kabla ya Mkurugenzi wa Ufundi wa Bologna, Giovanni Sartori, alipomnyatia.

Ilimchukua miezi 11 kabla msimu wa kwanza kamili wa Calafiori katika Ligi ya Serie A, kulimalizika kwa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya, kabla ya kuthibitishwa kuwa mchezaji bora wa Italia kwenye Euro 2024 na thamani yake sokoni kuongezeka mara 12.

Si wachezaji wengi kote barani Ulaya wanaweza kudai ongezeko kama hilo ndani ya kipindi kifupi kama hicho - na imemfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, kuhamia Arsenal kwa ada ya hadi pauni milioni 42 ikiwa ni pamoja na nyongeza.

### Je, Calafiori ni nani?

Calafiori amekuwa akizingatiwa kuwa mchezaji mwenye kipaji cha juu.

Roma ilipomuuza kwa euro 2.5 kwenda Basel miaka miwili iliyopita, walijumuisha kifungu cha asilimia 40 cha mauzo katika mkataba wake.

Kifungu cha asilimia 50 cha mauzo kilijumuishwa pia na Uswisi alipohamia Bologna kwa euro milioni nne mwaka mmoja baadaye.

Akiwa ameshinda jeraha baya la goti alipokuwa na umri wa miaka 16, na kukosa takriban mwaka mzima, Calafiori yuko imara kiumbo na ni mrefu.

Ni mchezaji mwenye nguvu ambaye anachukua fursa ya hatua zake ndefu uwanjani, lakini pia ni mzuri na mwenye kipaji cha kiufundi.

Ana nguvu angani na katika hali ya mtu mmoja-kwa mmoja, anageuka kuwa kiungo katika umiliki wa mpira, akipanda mita chache ndani ya uwanja na kusaidia kuwa kiungo mchezeshaji.

Anaona fursa zilizo wazi mbele yake na anajua jinsi ya kuziingia, kama vile pasi zake tano za mabao msimu uliopita zilivyothibitisha.

Akiwa na kipaji cha mguu wa kushoto, unaomwezesha kupiga pasi ndefu na za masafa mafupi, pale Bologna mara nyingi alivuka uwanja akitafuta winga wa kulia au kupiga pasi katikati ya uwanja ili kuwazidi wapinzani.

Calafiori ni mchezaji mahiri ambaye alikuwa kama beki wa pembeni wa kushoto.

Kocha wa zamani wa Bologna, Thiago Motta, mara moja alimweka katika nafasi ya kati zaidi ambapo angeweza kutumia muda wake mzuri, kuzuia mipira, kuwakabili wapinzani na kuanza kuanzisha mchezo kutoka nyuma.

"Tangu siku ya kwanza alipojiunga na Bologna, Thiago Motta, aliniambia angetumia uwezo wangu wote kama beki wa kati," Calafiori alisema Mei mwaka jana wakati wa mahojiano.

### Je, Calafiori atailetea nini Arsenal?

Bologna ilimaliza msimu huo kwa kushindwa mara sita pekee, ikiwa na safu ya tatu bora ya ulinzi katika Seria A nyuma ya Inter na Juventus - na sifa nyingi zinakwenda kwa Calafiori.

Muitaliano huyo sasa atalazimika kutafuta nafasi yake kwenye safu ya ulinzi ya Arsenal ambayo imekuwa safu ya ulinzi isiyoweza kupenyeka katika kampeni za mwisho za Ligi Kuu, ikiruhusu mabao 29 pekee.

Akilinganishwa na William Saliba, Gabriel Magalhaes na Ben White, Calafiori ana sifa tofauti.

Mchezo wake hufanya kazi vizuri timu inaposhambulia, lakini pia akisubiri fursa ya kufungua mchezo. Atawapa Gunners chaguo jingine la kuaminika wakati wanapoanzisha mchezo kutoka nyuma.

Anaweza kucheza upande wa kushoto au kama beki wa kati wa kushoto katika safu ya ulinzi ya watu wanne na pia safu ya nyuma ya watu watatu kama alivyofanya kwenye Euro 2024.

Calafiori amekuwa na msimu mmoja pekee katika kiwango cha juu zaidi cha soka, ambapo alianzishwa mara 26 katika Ligi Kuu akiichezea Rossoblu ambao walimaliza wa tano msimu uliopita.

Hata hivyo, hiyo ilitosha kumshawishi bosi wa Italia, Luciano Spalletti kumuanzisha katika mechi zote za Azzurri, ambapo alionesha umahiri wake na kuvutia klabu kubwa za Ulaya.

Kwa usaidizi wa Motta, Calafiori alifaulu bila tatizo hatua ya kuhamia kutoka Basel hadi Bologna.

Mikel Arteta atalazimika kumsaidia kufanya vivyo hivyo ikiwa anataka kupata ubora zaidi kutoka kwake London.

Ni hatua kubwa aliopiga na Muitaliano huyo atahitaji muda kuzoea. Kandanda ya Ligi Kuu ya Uingereza ina kasi zaidi kuliko Serie A, wachezaji wana muda mchache wa kufanya maamuzi na kucheza idadi kubwa ya mechi zinazohitaji sana nguvu kimwili.

Hata hivyo, Calafiori ana kila kitu kinachohitajika ili kufanikiwa: ujuzi mzuri wa kiufundi, maarifa, nguvu za kimwili, ujuzi wa mbinu na unyenyekevu.

Atafaidika na mtindo wa uchezaji wa timu yake mpya - inayocheza kama Bologna.

Kwa kiwango cha juu juu zaidi, taswira yake kwenye Euro ilifanana sana na ile ya watangulizi wengi mashuhuri wa Azzurri kama Paolo Maldini, Fabio Cannavaro na Alessandro Nesta, na hii haikuonekana bila kutambuliwa na wale wanaopenda urembo.

Na ikiwa taaluma ya Calafiori itakuwa sawa na watangulizi hao, waumini wa Gunners wanaweza kujigamba kwa miaka michache ijayo.

## Nukuu

"Tumekuwa na wiki tatu za maandalizi magumu kule Misri na tumerejea tumekutana na mechi ngumu ndio maana miguu ya wachezaji imekuwa migumu kufunguka hasa kipindi cha kwanza. Tumeiona Yanga ikicheza Afrika Kusini, itakuwa mechi ngumu (Ngao ya Jamii), lakini tutacheza kwa ajili ya kushinda," **Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, baada ya ushindi wa mabao 2-0 kwenye mechi ya Simba Days dhidi ya APR juzi.**




"Ilikuwa nzuri nilipozungumza naye mara moja au mbili na hapo ndipo sikujua kama tunaweza kufanya hivyo au la, alisisitiza - 'nijulishe ukiwa tayari, mikoba yangu iko tayari na ninataka tu kuja Arsenal' hayo yalikuwa maneno yake," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akilielezea namna beki wa kati Riccardo Calafiori alivyokuwa tayari kuondoka Bologna na kujiunga nao.**



"Nitaendelea sana kufunga kwa 'free kick' (faulo), tangu nikiwa Prisons nilikuwa nafanya hivyo na ninaendelea kufanyia mazoezi ili kila siku kuwa bora zaidi kwenye kupiga mipira ya adhabu, msimu uliopita sikupata nafasi ya kupiga free kick kwa sababu tayari kulikuwa na wapigaji," **Winga wa Simba, Edwin Balua, baada ya kufunga bao kali la mpira uliokufa kwenye mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya APR ya Rwanda juzi.**



# REKODI, TAKWIMU TAMU SIMBA DAY



Winga wa Simba, Edwin Balua, akishangilia bao la pili alilofunga kwa mkwaju wa faulo ya moja kwa moja, kwa staili ya kumbeba mwenzake Jean Charles Ahoua, huku wachezaji wengine wakionekana kuwakimbilia kwenda kuungana nao. Ilikuwa ni mechi ya Kilele cha Tamasha la Simba Day iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi, Simba ikishinda mabao 2-0 dhidi ya APR ya Rwanda. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba juzi ilifanya tamasha lake la 16 lililolibatiza jina la Simba Day, ambalo pamoja na mambo mengine ni kuwakutanisha wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwa ajili ya kufurahi pamoja, kupata burudani na kutambulisha kikosi cha msimu unaofuata.

**Simba ambao ndiyo waasisi wa matamasha hayo yaliyopigwa si tu hapa nchini bali na klabu nyingi kwa sasa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na Kusini, yaani CECAFA na COSAFA, walilifanya kwa mara ya kwanza 2009 chini ya Mwenyekiti wa wakati huo, Hassan Dalali na lengo lilikuwa ni kukusanya pesa kwa ajili ya kuendesha klabu bila kujua kuwa baadaye litakuwa moja kati ya tamasha kubwa Afrika.**

Kabla ya mchezo husika kulikuwa na burudani mbalimbali kutoka kwa wasanii wengi mashuhuri nchini, ikafuatiwa na michezo mbalimbali, kabla ya utambulisho wa wachezaji wote wa zamani na wapya, ambao watatumika kwa msimu ujao wa mashindano.

Wachezaji wapya wa Simba waliotambulishwa na wote walicheza ni Jushua Mutale, Steven Mukwala, Jean Charles Ahoua, Debora Fernandes Mavambo, Augustine Okajepha, Valentin Nouma na Karaboue Chamou, na Moussa Kamara ambapo wazawa ni, Abdulrazack Hamza, Valentino Mashaka, Omari Omari, Kelvin Kijili na Yusuph Kagoma.

Katika mechi hiyo, Simba ilishinda mabao 2-0 dhidi ya APR kutoka Rwanda, mabao yaliyofungwa na, Fernandes na Edwin Balua.

Nipashe limekusanya takwimu na rekodi za mechi hiyo ya juzi na Simba Day zilizopita...

### Ushindi mara 10

Ushindi wa juzi umeifanya timu hiyo kupata kushinda mara 10 ambapo mara ya kwanza ilikuwa 2009 lilipoanzishwa, ilipoifunga SC Villa ya Uganda bao 1-0, ikaitwanga tena SC Villa mabao 4-1 mwaka 2013 kabla ya kushinda tena timu hiyo hiyo ya Uganda bao 1-0 mwaka 2015.

Mwaka 2016 ikashinda mabao 4-0 dhidi ya AFC Leopards ya Kenya, ikaidungua Rayon Sport ya Rwanda bao 1-0 mwaka 2017, na kisha ikaishindilia Power Dynamos ya Zambia mabao 3-1 mwaka 2019, kabla ya kuifanyia mauaji Vital'O ya Burundi kwa mabao 6-0 mwaka 2020.

Kama vile haitoshi, ikashinda mabao 2-0 dhidi ya St George ya Ethiopia mwaka 2022, idadi kama hiyo ya mabao msimu uliopita dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, na mwaka huu ikashinda 2-0 dhidi ya APR ya Rwanda.

### Imepoteza mechi nne

Kati ya matamasha 16 iliyoyafanya, Simba imepoteza manne tu mpaka sasa, mara ya kwanza ikiwa ni 2011, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Victors FC ya Uganda, mwaka unaofuata 2012, ilikubali kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Nairobi City ya Kenya, na mara ya mwisho kupoteza ilikuwa ni 2021, ilipofunga bao 1-0 dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

### Sare mbili

Simba imetoka sare mara mbili tu katika mechi zake za tamasha la Simba Day, na mechi zenyewe zilikuwa ni dhidi ya Express ya Uganda mwaka 2010 na 2018 ilipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Asante Kotoko ya Ghana.

### Imecheza na SC Villa mara nyingi zaidi

Timu ambayo imecheza Simba Day mara nyingi zaidi ni SC Villa, ikifanya hivyo mara tatu 2009, 2013 na 2015 na mara zote timu hiyo ikiambulia kipigo dhidi ya Simba.

Timu nyingine ambayo imecheza mara nyingi dhidi ya Simba katika tamasha hilo ni Power Dynamos ya Zambia, ikifanya hivyo mara mbili mwaka 2019 na msimu uliopita.

### Mwaka wa tatu mfululizo ikishinda 2-0

Simba imepata ushindi wa mabao 2-0 kwa miaka mitatu mfululizo, tangu ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya TP Mazembe mwaka 2021.

Mwaka uliofuata 2022 ikaifunga St George mabao 2-0, na dozi hiyo ikaitoa pia kwa Power Dynamos ya Zambia mwaka jana, na mwaka huu kipigo kama hicho kimeenda kwa APR juzi.

### Wachezaji wapya wa kigeni moto

Katika Simba Day zote tatu ambazo imeshinda mabao 2-0, wachezaji wapya wa kigeni ambao wamekuwa wakiichezea timu kwa mara ya kwanza wamekuwa wakiwika kwa kufunga mabao.

Katika mechi ya juzi, mchezaji, Fernandes mwenye uraia pacha wa nchi za Congo Brazaville, lakini akiichezea Timu ya Taifa ya Gabon, alifunga bao la kwanza akiwa anaichezea timu hiyo kwa mara ya kwanza akisajiliwa kutoka Mutondo Stars ya Zambia.

Mwaka jana wachezaji Willy Onana na Fabrice Ngoma, wakiwa ndiyo kwanza wamesajiliwa, walifungia timu hiyo mabao mawili dhidi ya Power Dynamos, na 2022, Nelson Okwa alifunga bao la pili dhidi ya St George akiwa ndiyo kwanza amesajiliwa kutoka Rivers United ya Nigeria.

## JE, WAJUA?



Fulham wametangaza kumsajili kiungo wa Arsenal, Emile Smith Rowe, kwa dau lililoweka rekodi kwa ukubwa katika klabu hiyo, ambalo la awali ni pauni milioni 27. Ingawa 'Cottagers' hao hawajaweka wazi jumla ya ada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, inaeleweka kuwa mkataba huo unaweza kupanda hadi pauni milioni 34 pamoja na nyongeza.

# Wasimulia Mama Samia Legal Aid ilivyowakomboa

**Na Waandishi Wetu**

KAMPENI ya msaada wa kisheria ya Mama Samia imepiga kambi katika Maonesho ya Nanenane viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma.

Huku wananchi wakimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa msaada huo na kushauri iwe taasisi ya kudumu itakayowasaidia kupata haki zao kwenye migogoro ya kisheria.

Msaada huo unalenga kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu ya sheria, huduma za ushauri na ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ya kisheria wanayokumbana nayo katika maisha yao ya kila siku.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana walipofika kwenye banda hilo, walisema huduma hiyo imekuwa ni muhimu kwa wananchi kupata ufumbuzi wa migogoro inayowakabili.

Mkazi wa Kigamboni, Lameck Kipiliango alisema kampeni hiyo imekuwa msaada mkubwa kwa wananchi na kushauri Rais Samia aunde iwe taasisi ya kudumu kwa kuwa kampeni ina ukomo.

"Nimefika katika banda hili ili kusaidiwa kupata ufumbuzi wa mgogoro wake wa ardhi na Jiji la Dodoma, nimepata msaada wa kisheria nimeona kama ni Mungu aliniongoza nije hapa tunamshukuru sana mama (Rais Samia) ameleta kitu kipya huko nyuma hakikuwepo," alisema.

Alisema kampeni hiyo ikiundiwa taasisi kama ilivyo Taasisi ya Benjamin Mkapa itakuwa na uendelevu wa kutoa huduma hiyo kwa wananchi.

Mkazi wa Dodoma, Esther Lihofo alisema kampeni hiyo ni msaada kwa wananchi wasio na uwezo wa kuweka mawakili wanapotafuta haki zao mahakamani.

"Nimetembelea banda hili la sheria la Mama Samia nimekutana na ofisa anaitwa Koku amenipa ushauri na elimu nzuri kuhusu masuala ya kisheria najipanga vizuri kwenye kuweka mirathi, mpango huo ni mzuri katika kuwasaidia wananchi wasio na uwezo ambao hawana uwezo wa kuweka mawakili namshukuru sana Rais," alisema.

Mkazi wa Area C Dodoma, Thomas Peter, anasema amejifunza kupitia kampeni hiyo itasaidia wananchi wengi wasiokuwa na uelewa wa kisheria kuhusu masuala mbalimbali. Mkazi wa Hombolo, Lenard Hamis alisema amepata huduma nzuri kwenye banda la kampeni hiyo na amejifunza mambo ya kisheria ya kufuata na kutoa elimu kwa wananchi wenzao wa vijijini.

"Tumepewa namba za kupiga kwa ajili ya msaada wa kisheria tutawapa watendaji wasambaze kwa wananchi ili wanufaike na huduma hii ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, tunamshukuru sana Rais hakika mama anaupiga mwingi kwa wananchi wake,"alisema.

Mkazi wa Jiji la Dodoma, Yusuph Masatu, alisema amefarijika kupata huduma nzuri ambayo hakutegemea kuipa ya elimu ya masuala ya sheria.

"Nimshukuru Rais kwa kuona umuhimu wa kampeni hii, kweli watu ni wanyonge hawawezi kupata msaada wa kisheria kuwa na mawakili lakini ameliona hilo na kuleta kampeni hii ambayo itawasaidia sana watanzania tunashukuru sana," alisema.

**Imeandaliwa na Paul Mabeja (Dodoma), Elizabeth Zaya (Dar).**

# Nidhamu yaangusha vijana, wanawake sekta ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

BENKI ya NMB imesema ukosefu wa elimu ya fedha, nidhamu na kutosimamia malengo ni kati ya changamoto zinazokwamisha vijana na wanawake kupata mafanikio katika sekta ya kilimo.

Mratibu wa NMB Foundation, Thobias Mkamate amesema kwamba hiyo ndio siri ya taasisi hiyo kujikita zaidi katika kuelimisha makundi hayo kabla ya kuyakopesha.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Kongamano la Vijana na Wanawake kwa Maendeleo Endelevu ya Sekta ya Kilimo lililofanyika kwenye Maonesho ya Nanenane, jijini.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alikuwa mgeni rasmi wa kongamano hilo la kwanza katika Maonesho ya Nanenae, lililohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wakiwamo Wakuu wa Mikoa ya Dodoma na Singida pamoja na wakuu wa wilaya za mikoa hiyo, wakurugenzi na viongozi wastaafu.

Akizungumza na vijana na wanawake kutoka vyuo mbalimbali, taasisi za kilimo na vikundi vinavyojihusisha na mnyororo wa thamani wa kilimo, Mkamate alisema tofauti na taasisi nyingi za fedha ambazo haziamini katika makundi hayo, NMB imejikita kuyaelimisha ili yakopesheke na kurejesha.

"NMB tuna mikopo ya muda mfupi, yaani ya mwaka mmoja kama vile pembejeo za kilimo, vifaa vya uvuvi, ufugaji, mikopo ya kilimo cha mkataba; ya muda mrefu tuna mikopo ya uwekezaji ambayo inakupa mashine, matrekta, 'power tiller,' uchimbaji visima na ujenzi wa maghala.

"NMB tunatoa mikopo ya kilimo katika mnyororo mzima wa thamani, tangu unapoanzisha shamba, kupanda mbegu, kupalilia, kuvuna na kukuunganisha na masoko, lakini kwa vijana na wanawake tumekwenda mbele zaidi kwa kupitia NMB Foundation ambapo tunafanya mafunzo," alisema.

Mkamate alibainisha kwamba vijana wengi wakichukua mikopo, hawapeleki katika malengo husika waliyoyatumia kuomba mikopo, badala yake wanahamisha malengo hayo, jambo linalokwamisha ustawi wa shughuli zao, ndio maana kipaumbele ni kuwapa elimu na kuwaunganisha katika vikundi, sambamba na kuwapa elimu ya fedha.

Naibu Waziri Silinde alipongeza taasisi za fedha zikiongozwa na NMB kwa kuitikia kwa vitendo wito wa Rais Samia Suluhu Hassan kuzitaka benki kupunguza riba katika mikopo ya sekta ya kilimo hadi kufikia tarakimu moja.

"Tangu Rais Samia alipoingia madarakani, mikopo ya kilimo imeshuka na kuwa chini ya asilimia tisa, mkibisha nendeni NMB au katika benki zote, mwulize mtaambiwa haya yamefanikiwa kutokana na msukumo wa Rais na Wizara zake za Kilimo na ile ya Mifugo na Uvuvi," alisema.

Katibu Mkuu wa zamani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Philip Mangula, aliyehudhuria kongamano hilo aliwaeleza vijana na wanawake washiriki umuhimu wa sekta waliyochagua na kwamba siri ya mafanikio yao katika kilimo itatokana na nidhamu, ubunifu na kujitoa kwao.

Aliwataka kuzingatia mada mbalimbali zinazotolewa na watoamada ili kuhakikisha wanafanya kilimo chenye tija na kuepuka kilimo cha mazoea ambacho hakiwezi kuwapa mafanikio, huku akiwataka kutumia vyema fursa za mikopo ya taasisi za fedha katika kunyanyua uzalishaji.




Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara wa Benki ya NMB, Nsolo Mlozi (katikati), akihudumia wateja waliotembelea banda la benki hiyo katika Maonesho ya Kilimo ya Nane Nane yanayoendelea kwenye viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbegu za kahawa zinazostahimili magonjwa zazalishwa

**Na Valentine Oforo,**
DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI) imefanikiwa kuzalisha aina 23 za mbegu chotara zinazostahimili magonjwa ya kahawa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuboresha uzalishaji.

Miche hiyo ya mbegu iliyozalishwa katika misimu tofauti ya kilimo inajumuisha aina 19 ya kahawa ya arabica, fupi na ndefu, na nne za kahawa ya robusta.

Mafanikio hayo muhimu katika sekta ya kahawa nchini yamebainishwa jana jijini Dodoma na Grace Monyo, mzalishaji wa mbegu kitengo cha uboreshaji wa zao la kahawa wa TaCRI katika Maonesho ya 31 ya Kimataifa ya Kilimo Tanzania, Nane Nane.

Alisema kwa miaka mingi wakulima wa zao hilo la biashara nchini Tanzania wamekuwa wakikatishwa tamaa na magonjwa kadhaa sumbufu yanayoshambulia zao hilo, hali iliyopelekea baadhi yao kuachana na kilomo cha zao hilo.

"Magonjwa makuu yaliyokuwa yanawasumbua wakulima ni pamoja na ugonjwa wa chule buni na kutu ya majani, kwa upande wa kahawa ya arabica, na ugonjwa wa mnyauko fusari kwa kahawa ya robusta," alieleza.

Alisema kuzalishwa kwa aina hizo za mbegu chotara kumewahamasisha wakulima wengi kuanza tena kujihusisha na uzalishaji wa zao hilo katika mikoa mbalimbali.

Alizitaja baadhi ya mbegu hizo ndefu za chotara za kahawa ya arabica zilizozalishwa kuwa ni N39-1, N39-2, N39-3, N39-4, N39-5, N39-6, N39-7, KP423-1 , KP423-2, KP423-3, N39-8, N39-9, N39-10, N39-11 na N39-12.

"Aina za mbegu bora za robusta ambazo tumezalisha kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na tija ni Maruku 1, Bukoba 1, Maruku 2 na Muleba 1," alieleza.

Monyo alieleza kuwa TaCRI pia imezalisha mbegu za kahawa za arabica za compact, ambazo ni TaCRI 1F, TaCRI 3F, TaCRI 4F na TaCRI 6F.

Mbali na uwezo nzuri wa kukua vizuri, alisema aina hizo za mbegu zina ubora katika kuongeza tija na uzalishaji, kwani zinawawezesha wakulima kupata hadi kilo 5,000 kwa ekari.

Alisema uhitaji wa mbegu hizo umekuwa mkubwa sana miongoni mwa wakulima kupita uwezo wa uzalishaji wa taasisi hiyo.

Alisema TaCRI inashirikiana na vikundi vya wakulima na halmashauri zenye kilimo cha kahawa ili kuhakikisha miche ya mbegu hizo inazalishwa na kupatikana kwa wingi.





# Maaskari uhifadhi watakiwa kulinda maliasili

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

MAASKARI na maofisa wa Jeshi la Uhifadhi wanaofanya kazi kwenye hifadhi za taifa zilizoko katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wametakiwa kuongeza juhudi ya kulinda maliasili zilizoko kwenye hifadhi hizo ili ziendelee kulinufaisha taifa.

Pia, wametakiwa kuwalinda watalii wanapokuwa kwenye hifadhi hizo ili wawe salama na wanaporudi kwao wakawe mabalozi wa kuzitangaza maliasili na vivutio vilivyomo kwenye maeneo hayo.

Kamanda wa Uhifadhi wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Steria Ndaga aliyasema hayo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Askari wa Wanyamapori Duniani ambayo yalifanyika ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Alisema askari hao ndiyo nguzo ya ulinzi na usalama wa watalii na mali zao wawapo hifadhini pamoja na kuhakikisha rasilimali zilizomo ndani ya hifadhi hizo zinakuwa salama.

Alisema askari hao pamoja na wafanyakazi wengine wa shirika hilo wamekuwa wakifanya kazi nzuri ambayo imezifanya hifadhi hizo kuendelea kuwa salama licha ya baadhi ya changamoto ambazo zimekuwa zikiwakabili.

"Niwasisitize kwamba muendelee kufanya kazi kwa juhudi, nidhamu na kujitoa usiku na mchana ili maeneo yetu yaendelee kuwa salama na taifa liendelee kunufaika kwa kuingiza mapato yatokanayo na watalii na raslimali zingine zilizomo kwenye hifadhi hizi," alisema Steria.

Aliwasisitiza askari hao kuendelea kubuni mbinu za kukabiliana na majangili ambao wamekuwa wakizinyatia maliasili zilizomo hifadhini na kuziharibu akidai kuwa na wao wamekuwa wakibuni mbinu mpya za kuwakwepa askari hao.

Vilevile aliwataka maaskari hao kuwaombea wenzao ambao walipoteza maisha kwa nyakati tofauti wakiwa mstari wa mbele kulinda maliasili za taifa.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki alisema hifadhi hiyo imekuwa ikikabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu ikiwemo uingizaji wa mifugo ndani ya hifadhini.

Alisema maaskari wamekuwa wakifanya doria za ardhini na angani ili kuhakikisha maeneo yote ya hifadhi yanakuwa salama na kwamba wamekuwa wakichukua hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria wanapokamata mifugo hifadhini.

Aidha, alisema baadhi ya askari wamekuwa wakifanya kazi kwa kujitolea zaidi na hivyo akasema askari wanne waliofanya kazi vizuri wanapatiwa zawadi kama sehemu ya motisha kwao.

"Katika kutambua michango mbalimbali inayofanywa na askari, leo hii tumeandaa zawadi kwa baadhi ya askari walioonyesha umahiri katika kutimiza majukumu yao, zawadi tulizoandaa ni tuzo, vikombe na vyeti ambavyo tutakabidhi kwa maaskari wanne na ofisa mmoja," alisema Ole Meing'ataki.

Alisema maadhimisho ya askari wa wanyamapori duniani huwa yanafanyika kila mwaka kwa lengo la kuwakumbuka na kuwaenzi askari waliofariki ama kujeruhiwa wakati wakiwa wanatekeleza majukumu yao.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa askari wanyamapori 150 hufariki ama kujeruhiwa kila mwaka duniani wakitekeleza majukumu yao.

Maadhimisho hayo ya kanda yalifanyika kwa maaskari kushiriki kwenye michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Daniel Sillo akishiriki katika ujenzi wa kituo cha Polisi Nyamhongolo kilichopo wilayani Ilemela mkoani Mwanza wakati wa ziara yake ya siku mbili mkoani hapa mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mbunge wa Jimbo la Ilemela Dk.Angelina Mabula. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Walia ubovu Barabara Makambako-Mlowa

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WAKALA wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Njombe, umeombwa kutenga bajeti ili kujenga Barabara ya Makambako-Mlowa kulikojengwa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Makambako ili kuwaondolea wananchi kero ya ubovu wa barabara hiyo hasa wajawazito.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na baadhi ya madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Makambako wakati wa kikao cha baraza la madiwani cha kuishia robo ya nne ya mwaka wa fedha 2023/2024 kilichofanyika ukumbi wa Shule ya Sekondari Makambako.

Madiwani hao walisema barabara hiyo imeharibika na inahatarisha maisha ya wagonjwa hasa wanawake wajawazito ambao wanafuata huduma za afya katika hosptali hiyo.

Mmoja wa madiwani hao kutoka Kata ya Mlowa, Odilo Fute alisema barabara ya kwenda Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Makambako haipitiki.

"Hili ni tatizo kubwa mh. mwenyekiti hili eneo la Darajani kwenda kule hospitali wagonjwa wanapata shida sana, namna ya kwenda kule wajawazito wanateseka mno siyo kidogo," alisema Fute.

Diwani wa Kata ya Makambako, John Ngimbuchi alisema endapo barabara hiyo haitatengenezwa itasababisha adha kwa wajawazito kujifungulia njiani hata kupoteza maisha.

"Ahadi zimekuwa ahadi kwa kweli wenzenu tunalaumiwa sana kuhusu hii barabara kwa sababu imekuwa na hali mbaya," alisema Ngimbuchi.

Naye aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Imani Fute aliwataka TARURA kuona namna ya kufanya marekebisho barabara hiyo ya kuelekea hospitali kwa sababu imekuwa na watumiaji wengi kwa sasa.

Meneja Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Njombe, Costantine Ibengwe alisema katika mwaka huu fedha wamepata fedha ambazo zitumika kujenga mfereji wa maji taka katika mtaa wa Kitisi na kueleza kuwa watendelea kuomba fedha serikalini ili kuona namna ya kufanyia matengenezo barabara zenye matatizo.

Ibengwe alisema tayari wameshaifanyia tathimini Barabara ya Makambako-Mlowa ambapo mwaka wa fedha 2024/25 wametenga kilometa moja kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami pamoja na matengenezo mengine katika maeneo korofi.

# Diwani awafunda wananchi kuelekea uchaguzi S/mtaa

**Na Christina Mwakangale,**
MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Utengule-Usongwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameaswa kuepuka kurubuniwa kwa kupewa zawadi ndogo ndogo na wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Badala yake wametakiwa wachaguwe viongozi wenye uwezo wa kutatua shida zao.

Diwani wa kata hiyo, Yona Ntunjilwa aliyasema hayo mkoani Mbeya, wakati tukio la kuwakabidhi watoto, wajane na wagane wa kata hiyo, msaada wa nguo lililoandaliwa na Shirika la Sauti ya Mama Afrika Foundation (SAMAFO), kwa kushirikiana na wadau.

"Mwaka huu tuna uchaguzi wazee msirubuniwe huko nje kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Wazee mjitokeze kupiga kura ya maoni na kura yenyewe," alisema Ntunjilwa na kuongeza.

"Kinamama nyie mna nguvu sana na usipowasemea yanayowahusu, umekwenda na maji. Wanawake wanaweza bila kuwezeshwa," aliongeza.

Njunjilwa aliwawakumbusha viongozi wenzake kwenye kata hiyo, kutambua mahitaji ya wakazi wao, kwa kuwatembelea huku akiwataka waliopewa msaada huo kuwa shukrani hata kama ni kidogo.

"Viongozi wa mtaa mnatakiwa kujua hali ya maisha ya wakazi wenu na kuweka utaratibu wa kutoa msaada hasa kwa wajane na wagane. Wazee kwenye jamii ni muhimu huonya, hufundisha.

"Tumejifunza leo kutokana na msaada wenu huu, uliotolewa kutoka kwa wadau na wenzetu na kuwakumbuka wakazi wa eneo letu. Ukiwatazama wazee hawa utabaini ni kati ya wanaohitaji msaada," aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa SAMAFO, Tabitha Bugali, alisema utaratibu wa kutoa msaada kwa makundi maalumu kama vile yatima na wazee ni endelevu, kwa kushirikiana na wadau wengine wenye malengo yanayofanana.

"Tumeshirikiana na wenzangu kutoka shirika la AMAWAMBE, Twende Wote Foundation (TWF), pamoja na Mary Gumbo, kutekeleza jambo hili ikiwa ni miongoni mwa shughuli tunazofanya kuigusa jamii," alisema Tabitha.

Mary Gumbo, aliyekuwa mkuu wa dawati la jinsia Jeshi la Polisi Mbeya DC na kata hiyo, alisema kutoa msaada kwa kundi hilo ni kumshukuru Mungu kudumu kazini kwa miongo kadhaa, hadi kustaafu Julai mwaka huu.



## Katibu Mkuu ahimiza matumizi teknolojia mifugo, uvuvi

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe, amehimiza matumizi ya teknolojia ya mifugo na uvuvi kwa wafugaji ili kuweza kuleta tija katika uzalishaji.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea maonesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa mkoani Dodoma, alisema katika maonyesho hayo kuna teknolojia nzuri ya ufugaji na uvuvi kwa hiyo wafugaji na wavuvi wanapaswa kufika kuchukua teknolojia hiyo ili kuboresha mifugo yao.

"Mnakumbuka Waziri Mkuu Kassim Majaliwa jana alisema maana halisi ya haya maonesho ni kwamba wakulima waje kuchukua teknolojia" alisema Prof. Shemdoe.

Aidha, Prof. Shemdoe alisema maonyesho hayo ni kwa mara ya kwanza yanaadhimishwa kimataifa mkoani Dodoma na ameweza kutembelea mabanda mbalimbali ya mifugo na uvuvi pamoja na kilimo ikiwa na sehemu ya vipando.

Vilevile Prof. Shemdoe alitoa wito kwa Watanzania kutumia siku nane kutembelea maonesho haya ya nanenane ili kujionea teknolojia mbalimbali zinazopatikana ambazo zitawasaidia katika shughuli za uzalishaji.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alimshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kutembelea maonesho hayo.

Vilevile, Jabir alisema maonesho haya yatawasaidia wananchi wa Tanzania kubadirisha maisha yao kwa kuongeza kipato na kukuza uchimi wa nchi, kwani elimu wanayoipata kwenye maonesho haya yatakuwa na maboresho na mapinduzi makubwa kwao.

# Dk. Mwinyi: Kilimo kimechangia 24% pato la taifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema sekta ya kilimo Zanzibar kwa mwaka 2023 imechangia asilimia 24.6 katika pato la taifa.

Amesema endapo sekta hiyo itafanya vizuri zaidi katika uzalishaji wa chakula na biashara itakuwa na mchango mkubwa zaidi katika uchumi wa nchi.

Alisema hayo wakati akifungua maonyesho ya kilimo (Nanenane) Dole visiwani Zanzibar, alisema mapinduzi ya kilimo ni jambo la msingi na lakupewa kipaumbele kwa sababu kwa muda mrefu sekta hiyo haijatoa matokeo halisi yanayotarajiwa.

Alisema serikali imedhamiria kuleta mageuzi hayo ili kukifanya kilimo kiwe cha biashara na chenye tija.

Dk. Mwinyi alisema lengo la mageuzi hayo ni kukibadilisha kilimo kilichozoeleka na kukifanya kiwe cha tija ambapo mageuzi hayo yatabadilisha mnyororo wa thamani kutoka shambani hadi kufika kwa mlaji.

Kadhalika alisema sekta hiyo inaunganisha sekta nyingi muhimu, ikiwemo ya biashara na viwanda, utalii, maji na nishati, hivyo ikifanya vizuri italeta matokeo chanya kwa uchumi wa nchi.

"Juhudi hizi ni za lazima ambapo kila mdau anatakiwa kushiriki kikamilifu katika kuunga mkono adhma ya kuleta mageuzi haya" alisema Rais wa Zanzibar.

Alisema Zanzibar kuna ongezeko la kilimo cha mbonga na matunda na takwimu zinaonesha kuna ongezeko kwa mazao hayo kutoka tani 66,304 mwaka 2022 hadi tani 87,971 mwaka 2023.

Dk. Mwinyo alisema matokeo ya hatua hiyo yamesababisha kupungua kwa utegemezi mkubwa wa mazao ya matunda na mboga kutoka Tanzania Bara.

Aidha, alisema kilimo hicho kinajumuisha zaidi vijana na wanawake na kinaleta matokeo chanya ya ongezeko la ajira na kwamba serikali inatarajia kuazisha kituo maalum kwa kila wilaya ili kurahisiha upatikanaji wa huduma za kilimo kwa wakulima na wafugaji.


Akizungumzia kuhusu mifugo, Dk. Mwinyi alisema serikali inatarajia kutekeleza mradi mkubwa wa mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo ambao utazingatia mabadiliko ya tabianchi ambapo mradi huo unathamani ya Sh. bilioni 7.5.

Dk. Mwinyi alisema mradi huo unalengo la kuleta mageuzi ya mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa maziwa kwa ajili ya kukuza hali ya maisha ya jamii na kuimarisha uhakika wa chakula na lishe.

Hivyo, aliwataka vijana kuitumia fura zilizopo katika sekta ya kilimo na mifugo kwa kujiajiri na kuyatumia maonesho hayo kwa kujifunza mbinu bora za kilimo na ufugaji, kwamba serikali ipo tayari kuwasiadia katika kuleta mageuzi ya kilimo na mifugo.

Naye Waziri wa Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema maonyesho hayo yametoa fursa kwa wajasiriamali wa kilimo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ali Khamis alisema juhudi za pamoja ikiwemo za wadau zimewezesha kufanyika kwa maonesho hayo yaliyoshirikisha washiriki 300.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Zanzibar, Dk Muingereza Miraji (katikati waliokaa), Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu Zanzibar, Hamad Hamad (wapili kulia waliokaa), Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Dk Ally Possi (wapili kushoto waliokaa) na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Abdallah Mitawi (wakwanza kushoto waliokaa) wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya kikao cha pamoja cha kujadili changamoto za taasisi zilizo chini ya wizara hizo. **PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

# Makamu wa Rais awapa somo watatuzi kero za muungano

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka viongozi wanaoshughulikia masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kujadili kwa kina na bila woga masuala yote magumu yanayohusu muungano, ili waweze kuyapatia ufumbuzi wa uhakika.

Alisema hayo ofisini kwake Migombani Mjini Zanzibar alipokutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Dk. Ashatu Kijazi aliyefika ofisini kwake, kujitambulisha baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo hivi karibuni.

Othman alisema kumejengeka dhana kwa baadhi ya viongozi kwamba yapo baadhi ya masuala yamuungano ambayo hayawezekani kuzungumzwa, jambo ambalo litanaendelea kuleta shida kwenye muungano huo.

Alisema kuna dhana kwamba kila mmoja miongoni mwa viongozi anahitaji kuonekana kwamba yupo sawa kisiasa na kuacha uhalisia kwenye masuala na kero za muungano jambo ambalo linaweza kuharibu jitihada za kutatua kero za muungano huo.

Pia, aliwataka viuongozi wote wanaoshughulikia muungano kuwa wakweli katika kuzungumzia uhalisia wa masuala yanayoleta changamoto kati ya pande mbili za muungano, kwa kuyakabili, kuyainisha na kuyazungunza bila woga na hatimaye kuyapatia ufumbuzi.

Alitaja mfano wa mafuta na gesi asilia, Bandari na leseni za viwanda, Tume ya pamoja ya fedha kwamba ni mambo yaliyoandikwa na kuainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Waziri Dk. Kijazi aliahidi kwamba wizara yake itajitahidi kushirikiana na pande mbili za muungano katika kuyajadili masuala yaliyopo kwenye muungano yanayoleta kero miongoni mwa washirika wa muungano huo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**HUSNA YAHYA SWALEH** anatangaza kupotea kwa vyeti vya kidato cha nne vyenye index namba **S.1357/ 0003/2016** na **P.0725/0023/2017** vilivyotolewa na baraza la mitihani la taifa **AHLLILBAYT ISLAMIC CENTER na NEWMAN SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016 na 2017. Pia kapoteza cheti cha cha kidato cha sita chenye index namba **S.4862.0507.2020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia GOMBE HIGH SCHOOL mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/PWA/KIS/15156/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AZIZ S KIRONGOMARA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA STARLET RANGI NYEUSI YENYE USAJILI **T 524 AXS** CHASISI NAMBA:**EP910278248** KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/11525/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAMZA ABDALLAH MCHUCHURI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER 125** yenye usajili namba **MC 866 DPS**, chassis namba : **MD2B15BX7NWF94777** na engine namba: **JVXWNF28793.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/UBU/15940/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IMANI N ULOMI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA HILUX yenye usajili namba **T 642 ABZ**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

POLISI TAARIFA: **PHQ/-DAE/KIN/160858/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU MSAFIRI RAFAEL KAMATE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 887 ACD** aina ya ***FEKON.*** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **PHQ/DOD/DOD/31948/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**PRIME POWER TANZANIA LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi za magari zenye namba za usajili **T 270 EEJ na T 271 EEJ** zote aina ya **TOYOTA HILUX (PICK-UP).** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/157142/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PRISCA PROSPER CHACHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 500 BUM** aina ya **TOYOTA NOAH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/135512/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VENANCE EMMANUEL KIMARIO** anatangaza kupoea kwa kadi ya pikipiki yenye jina la umiliki **MOHAMMED ENTERPRISES (T) LTD** aina ya BAJAJI BOXER yenye usajili namba **MC 157 DTP**, CHASSIS NAMBA : **MD2B15BXSN-WJ95959** na ENGINE NAMBA: **JVXWNJ46761**.Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DOD/-DOD/32825/2024**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 15975 YA MWAKA 2024.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU LADISLAUS MWALIMU SALEMA**

**PETER LADISLAUS SALEMA ....MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 15 mwezi wa NANE, 2024, saa 2.30 asubuhi. Siku ambayo shauri limepangwa kusikilizwa Mbele ya Mhe Jaji M. MNYUKWA.

Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 25 mwezi wa Julai, 2024.

**NAIBU MSAJILI**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI SUB- REGISTRY**
**AT MOSHI**
**MISC.CIVIL APPLICATION NO.7913 OF 2024**

(C/F Misc. Application N0. 282 of 2020: Originally from Judgment & Decree in the Application No. 04/2015/of the District Land and Housing Tribunal for Moshi at Moshi)

IDRISA YUSUPH MSANGI.................................APPLICANT
VERSUS
ZENA BAKARI MBWAMBO........................................1st RESPONDENT
MWAJUMA TWALIB RAMADHANI..........................2nd RESPONDENT

TO: ZENA BAKARI MBWAMBO.

NOTICE FOR RULING,

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for ruling in the High Court of Tanzania at Moshi on 21st day of August, 2024 at 9:00 a.m. before Honourable **L. M. MONGELLA,** judge.

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe Newspaper .

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 26th day July ,2024

DEPUTY REGISTRAR

**KATEMANA AUCTION MART & GEN. SUPPLIES**
(Auctioneers. Brokers. Debt Collectors. Estate Agents & Commission Agents)
WAPAMBANAJI

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na Chama cha Ushirika **KAIGARA LIVESTOCK COOPERATIVE SOCIETY LIMITED** tutauza kwa mnada wa hadhara mali za chama hicho zilizo orodheshwa hapa chini.

| NA | JINA LA MMILIKI | MALI INAYOUZWA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | CHAMA CHA USHIRIKA KAIGARA LIVESTOCK COOPERATIVE SOCIETY LTD | VIWANJA 2 NA NYUMBA VYENYE HATI | ENEO LA VIWANDA KARIBU NA MAI JUICE | **17/08/2024 SIKU YA JUMAMOSI SAA 5.00 ASUBUHI** |

**MASHARITI YA MNADA: -**

1. Mnada utafanyikia sehemu mali ilipo na itauzwa kama ilivyo.
2. Mshindi wa mnada huo atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei itakayofikiwa na aslimia Sabini na tano (75%) italipwa ndani ya siku kumi na nne (14). kuanzia tarehe ya mnada, Endapo mteja atashindwa kumalizia ndani ya siku hizo mnada utarudiwa na pesa aliyotoa haitarejeshwa,

**Kwa mawasiliano piga simu zifuatazo:-**
*Mkurugenzi Katemana Auction Mart:-*
**Mob. 0763 452 525 / 0715 756 567**
Au fika ofisi za Afisa Ushirika Wilaya ya Muleba kwa ufafanuzi zaidi

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie, 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Naibu Spika anusuria ajali ya helikopta

**KAMPALA,** Uganda

NAIBU Spika wa Bunge la 11 la Uganda, Thomas Tayebwa amenusurika kifo baada ya helikopta aliyokuwa akiitumia kusafiria kuhusika katika ajali mbaya.

Ilielezwa kuwa ajali hiyo ilitokea juzi na kwamba Tayebwa yuko sawa na kila kitu alichokuwa amesafiri nacho ikiwemo wasaidizi wake.

Chapisho aliloweka kwenye mtandao wa kijamii wa X jana Tayebwa alisema "Wapendwa, mimi na wenzangu tuko sawa. Hakuna aliyeumia".



Pia ilielezwa kuwa Tayebwa Jumamosi alihudhuria hafla ya serikali huko Nebbi, Nile Magharibi, na alisafiri hadi Bushenyi kwa Helikopta hiyo ili kuwapigia debe Edinah binti wa Mkuu wa Shirika la Taifa la Majisafi na Majitaka (NWSC), Injinia, Silver Mugisha, na Annet Katusiime Mugisha Mbunge wa Bushenyi Mwanamke.

Ajali hiyo inaripotiwa kutokea akiwa njiani kurejea Kampala kutoka Bushenyi, kwa mujibu wa ripoti ambazo bado hazijathibitishwa. **BBC**



Vikosi vya usalama vya Nigeria vikirusha gesi ya kutoa machozi kuwatawanya waandamanaji wakati wa maandamano, juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Samia apongeza kampuni iliyojenga reli ya kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amepongeza kampuni ya Yapi Merkezi, mkandarasi mkuu wa mradi wa reli ya kisasa ya umeme (SGR) kati ya Dar es Salaam na Dodoma kwa mchango wake katika maendeleo ya Tanzania.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo Alhamisi iliyopita, Rais Samia alisema mafanikio hayo yaliyoongozwa na Yapi Merkezi, yatasaidia kuongeza usafiri na kuchochea maendeleo.

Alisema hatua hiyo inaashiria enzi mpya ya kuunganishwa, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kiteknolojia kwa nchi.

"Mradi huu ni ushahidi wa uwezo wa kipekee na taaluma ya Yapi Merkezi. Juhudi zao na kufuata viwango vya juu zimefungua njia kwa ajili ya mustakabali mzuri zaidi kwa taifa letu.

"Reli ya SGR itakuwa na jukumu muhimu katika safari yetu kuelekea ustawi wa kiuchumi na ujumuishaji wa kanda," alisema.

Reli hiyo inatarajiwa kuboresha ufanisi wa usafiri, kupunguza muda wa safari na kuhakikisha usafiri wa bidhaa na abiria kwa urahisi na uaminifu zaidi.

Mradi wa SGR uliofanywa na Yapi Merkezi Insaat ve Sanayi Anonim Sirketi, ulijumuisha kubuni na kujenga sehemu muhimu kutoka Dar es Salaam hadi Isaka, ukifunika zaidi ya kilomita 1,000.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli la Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa pia alishukuru kampuni hiyo na SGR inadhihirisha nguvu ya ushirikiano wao na kampuni hiyo.

Makamu wa Rais wa Yapi Merkezi, Dk. Erdem Arioglu, alishukuru uongozi wa Tanzania na TRC kwa msaada wao wa karibu.

## Marathon ya CRDB yakusanya Dola 50,000 kusaidia wodi ya watoto DRC

**LUBUMBASHI,** DRC

CRDB Bank Marathon imefanyika kwa mara ya kwanza nje ya mipaka ya Tanzania katika Jiji la Lubumbashi, zaidi ya wakimbiaji 1,000 wakishiriki na kufanikisha lengo la kukusanya Dola za Marekani 50,000 kwa ajili ya kusaidia wodi ya watoto katika Hospitali ya Jason Sendwe.

Mgeni rasmi katika mbio hizo ambazo zimeweka historia katika marathon zilizowahi kufanyika katika Jiji la Lubumbashi, alikuwa Gavana wa Jimbo la Haut-Katanga, Jacques Kyabula ambaye aliambatana na mawaziri 10 wa jimbo hilo wakiongozwa na Waziri wa Michezo pamoja na Waziri wa Afya.

Viongozi hao pia waliambatana na Balozi wa Tanzania DRC, Said Mshana, Balozi wa Burundi DRC pamoja viongozi mbalimbali wa Benki ya CRDB wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Bruce Mwile.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mbio hizo za hisani zilizobeba kaulimbiu 'Tabasamu Limevuka Mipaka', Gavana Kyabula alipongeza Benki ya CRDB kwa kuwaleta pamoja raia wa Congo pamoja na washiriki kutoka mataifa ya jirani kuchangia kuboresha huduma za afya kwa watoto na kukuza ustawi wa jamii.

"Tunaishukuru CRDB Bank Marathon kwa kusaidia jitihada za serikali kuboresha huduma za afya kwa wananchi. Serikali yetu inatoa kipaumbele kikubwa katika afya, na tunafurahishwa na jitihada zinazofanywa na Benki ya CRDB katika kusaidia kuboresha afya ya watoto," alisema Gavana Kyabula.

Balozi wa Tanzania DRC, Balozi Said Mshana alipongeza Benki ya CRDB kwa juhudi zake za kukuza uhusiano wa kimataifa na kuimarisha umoja na mshikamano katika jamii.

Balozi Mshana alisema mbio hizo zilizozaliwa Tanzania zinaonesha ubunifu ambao taasisi za kitanzania zinaweza kupeleka nje ya nchi katika kusaidia kukuza ustawi wa jamii.

Mwenyekiti wa Bodi ya CRDB Bank DRC, Dk. Fred Msemwa alieleza kuwa marathon hiyo ni sehemu ya mkakati wa benki kusaidia juhudi za serikali katika kukuza ustawi wa watu wa Congo.

Akitangaza matokeo ya mbio hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Congo, Jessica Nyachiro, alishukuru washirika wa mbio hizo Africell, Orange, Ogowe Cleaning, Kin Marche, Policlynique Delta, Shalina, Vinmart Foundation, SUNU Insurance na Dukan.

"Pamoja na kuwa huu ni mwaka wa kwanza kwa mbio hizi lakini mwitikio umekuwa mkubwa sana. Tunawashukuru sana washirika wetu na wakimbiaji wote mlioungana nasi kusambaza tabasamu kwa watoto," alisema.

Marathon iliyofanyika leo Lubumbashi ni ya kwanza kati ya tatu ambazo zimepangwa kufanyika mwaka huu DRC, Burundi, na Tanzania. Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation ambao ndio waandaji wa mbio hizo, Tully Esther Mwambapa alieleza furaha yake baada ya mbio hizo zilivyopokelewa vizuri DRC.

Tully alishukuru Watanzania ambao wamejitokeza kwa wingi kushiriki mbio hizo za DRC, pia washirika wakuu wa mbio hizo, wakiwamo Sanlam, CRDB Insurance Company.

# SHOLO MWAMBA, BARAKA THE PRINCE KUPAMBA PAMBA DAY

**Na Adam Fungamwango**

WASANII Sholo Mwamba na Baraka The Prince, wanatarajia kupamba Kilele cha Tamasha la Klabu ya Pamba litakalofanyika Jumamosi ijayo Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Sholo ambaye ni mwimbaji wa muziki wa singeli, na Baraka, wote wawili wamethitisha kuwapo Mwanza siku hiyo kwa ajili ya kutoa burudani na kukitambulisha kikosi kipya siku hiyo iliyopachikwa jina la Pamba Day.

Pamba itakipiga na Vital'O ya Burundi katika mechi ya kilele cha tamasha hilo, ambapo kabla kutakuwa na burudani mbalimbali.

**Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, amewataka mashabiki wa mkoa huo na jirani kujitokeza kwa wingi na matarajio yao ni kuujaza uwanja.**


"Hii ni Wiki ya Pamba, kabla ya kilele tutakuwa na shughuli mbalimbali za kijamii, pamoja na kuzidua jezi mpya za klabu na kuanza kuziuza rasmi," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Pamba Day, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alisema maandalizi kabambe yamefanyika, na yanaendelea kufanyika kwa ajili ya tamasha hilo, huku akibainisha kuwa wamesajili kikosi kabambe ambacho kitakuja kuleta ushindani.

Pamba itacheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ikiwa ni mara ya kwanza baada ya miaka 23, kwani ilishuka daraja mwaka 2001, na majaribio kadhaa ya kutaka kurejea yalishindikana mpaka ilipofanikiwa msimu huu.

Baadhi ya wachezaji wapya ambao imewasajili ni James Mwashinga, Samuel Antwi, Kelvin Nyanguge, Ally Ramadhani Juma, Paulin Kasindi, Paul Kamtewe, Christopher Oruchum, Kenneth Kunambi, Mukenya Alain, Yunus Lema, Costantino Almisu, Salehe Masoud, Erick Okutu na wengineo.

**UDHAMINI...**




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Manzi Rwegasira (katikati) na Mkuu wa Kitengo cha Makampuni Makubwa wa benki hiyo, Ester Manase (kushoto), wakikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 15, kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wafanyabiashara wa China nchini, Shi Yong (kulia), kwa ajili ya udhamini wa mashindano ya 11 ya mpira wa kikapu ya wafanyabiashara wenye asili ya China. Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika viwanja vya Starlight Arena jijini Dar es salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Wanne wafuzu fainali za KCB East Africa Golf Tour*

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI wanne wa mchezo wa gofu, wamefuzu kushiriki fainali za Mashindano ya KCB East Africa Golf Tour zitakazofanyika Desemba mwaka huu, Nairobi nchini Kenya.

Wachezaji hao wamepatikana kupitia shindano la wazi la KCB East Africa Golf Tour, lililomalizika juzi kwenye viwanja vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania JWTZ, Dar es Salaam..

Wachezaji hao ni Peter Mlewi ambaye ndiye bingwa wa shindano hilo kwa mwaka huu baada ya kupata pointi 42, akifuatiwa na Meja Jenerali Ibrahimu Muhona, aliyejikusanyia pointi 41, huku nafasi ya tatu ikienda kwa Khadija Seleman mwenye pointi 40, akifuatiwa na Hawa Wanyeche aliyekusanya pointi 39.

Akizungumza katika hafla ya kufunga shindano hilo jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi wa Benki ya KCB, Cosmas Kimario, aliwapongeza washindi waliofanikiwa kupata nafasi ya kwenda kuiwakilisha Tanzania katika shindano hilo nchini Kenya.

Alisema KCB itagharamia safari za wachezaji hao ikiwamo malazi, na kudai mshindi atakayepatikana katika fainali hizo atazawadiwa fedha.

"Tunashukuru Mungu kwa kumaliza salama nakupata washindi wetu ambao watakwenda kupambana na hatimye kurudi na ushindi," alisema Kimario.

Naye Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, aliwapongeza wachezaji hao na kuwataka kwenda kuipeperusha vema bendera ya Taifa.

"Ninawapongeza washindi wote ambao wamepata fursa ya kwenda kushiriki fainali za mashindano haya nchini Kenya, vile vile Benki ya KCB kwa kuendesha shindano ambalo limefana kwa kiasi kikubwa, alisema Ndumbaro.

Aliomba wadau wengine kujitokeza kusaidia mchezo huo hususan kwa upande wa kuinua vipaji vya vijana wanaochipukia.

Kuanzia mwakani gofu itachezwa UMISSETA na UMITASHUMTA na tayari viongozi wa gofu nchini wameanza maandalizi, hivyo wanaombwa kuungwa mkono kwa jambo hilo kwa kuziandaa timu hizo vizuri kuelekea katika mashindano mbalimbali.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Klabu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, aliwapongeza wachezaji hao kwa kuonyesha umahiri na kuwataka wale ambao hawajapata nafasi hiyo waendelee kufanya mazoezi zaidi.

Alibainisha kuwa wapo tayari kuendesha shindano lolote katika viwanja hivyo na kuwataka Watanzania kuendelea kushirikiana nao.

# Prisons kurejea Mbeya tayari kwa Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Tanzania Prisons leo inatarajia kurejea nyumbani Mbeya kwa ajili ya maandalizi ya ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ambao unatarajiwa kuanza rasmi Agosti 16, mwaka huu.

Prisons iliweka kambi yake jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

Ofisa Habari wa Tanzania Prisons, Chacha Waisaka akizungumza na gazeti hili jana, alisema wapo tayari kucheza na yeyote katika ligi hiyo kwa kuwa wamejiandaa vizuri.

Alisema wana kikosi kizuri na kipana na wameongeza wachezaji wawili wa kuongeza upana wa kikosi na ubora ambao ni Vedastus Mwahambi na Ezekiel Mwashilindi.

"Kambi imemalizika na imekuwa na mafanikio kwa sababu tumefanya 'sesheni' zote ambazo mwalimu alizokuwa anazihitaji kwa mchezaji," alisema Waisaka

Alibainisha kuwa wamefanyia mazoezi ya ufukweni, gym, barabarani, kucheza michezo ya kirafiki ya kujipima nguvu, ambavyo vimemfanya mchezaji awe kamili na fiti.

Aliongeza, "mwalimu Mbwana Makata amefurahi kwa sababu tumepata kile alichokuwa anakihitaji ili mchezaji kuwa fiti.

Aliwaomba mashabiki wa Prisons kurudisha imani kwa timu hiyo na kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani ili kuiunga mkono kwani lengo lao ni kuhakikisha wanashiriki michuano ya kimataifa msimu ujao jambo litakalorudisha heshima kwa timu hiyo.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ALVAREZ ANUKIA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid ipo kwenye mazungumzo na Manchester City kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wao wa Argentina, Julian Alvarez, mwenye umri wa miaka 24. ***(Athletic)***

### ARSENAL NAO WAMTAKA

ARSENAL pia inafikiria kumnunua Julian Alvarez, lakini 'Washikabunduki' hao huenda wakalazimika kuwauza wachezaji zaidi ili kufadhili ununuzi wake. ***(Mirror)***

### GUEHI ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle inatumaini kufanikisha mpango wa kumnunua beki wa England na Crystal Palace, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

### BEI YA SOLANKE HII HAPA

KLABU ya Bournemouth imesisitiza kwamba Tottenham Hotspur italazimika kutimiza masharti yao ya pauni milioni 65 ikiwa msimu huu wanataka kumsajili mshambuliaji wa England, Dominic Solanke, 26. ***(Mirror)***

### TODIBO AKARIBIA JUVENTUS

KLABU ya Jventus inakaribia kumnunua mlinzi wa Nice na Ufaransa, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 24, ambaye hapo awali alikuwa akihusishwa na Manchester United na West Ham. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### KOOPMEINERS AKOMALIWA

JUVENTUS itarejea Atalanta na ofa yao iliyoimarishwa ya euro milioni 55 kwa ajili ya kiungo wa Uholanzi, Teun Koopmeiners, 26. ***(Corriere dello Sport)***

### NKETIAH BEI JUU ARSENAL

ARSENAL inataka pauni milioni 30 pamoja na kipengele cha mauzo kilichojumuishwa katika mkataba wowote wa kumuuza mchezaji wa Kimataifa wa England, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 25, huku Marseille wakimnyatia mshambuliaji huyo. ***(Fabrizio Romano)***

### SOLER ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inataka kukamilisha dili la pauni milioni 13 na Lanus kwa ajili ya beki wa kimataifa wa Argentina, Julio Soler, ambaye wanamuona kama mbadala wa muda mrefu wa beki wa Scotland, Andrew Robertson, 30. ***(Sun)***

### MATETA ATAKA MKATABA

JEAN-Philippe Mateta mwenye umri wa miaka 27, ana nia ya kusaini mkataba mpya na Crystal Palace huku RB Leipzig na Napoli zikiwa na mpango wa kumnunua mshambuliaji huyo wa Ufaransa. ***(Sun)***

### WALKER-PETERS KUBAKIZWA

KLABU ya Southampton inatumaini kuwa itafanikiwa kumbakiza mlinzi, Kyle Walker-Peters, 27, katika klabu hiyo msimu huu baada ya West Ham kujiondoa katika mazungumzo ya kumsajili. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KOCHA AIONYA BARCA KUHUSU KUMSAJILI OLMO

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa RB Leipzig, Marco Rose, ameionya Barcelona kwamba ni lazima waimarishe ofa yao iwapo wanataka kuishawishi klabu hiyo kuachana na kiungo Dani Olmo.

**Wakati maslahi binafsi yameripotiwa kuwa tayari yamekubaliwa kati ya Barcelona na Olmo, bado kuna kazi kubwa ya kufanywa kuhusu ada ya uhamisho.**

Barca wanasemekana kuwasilisha ofa yenye thamani ya euro milioni 61, lakini kwa mpango wa malipo ambao umeiacha Leipzig bila kufurahishwa.

Akijibu ofa ya Barcelona, Rose aliviambia vyombo vya habari: "Mchezaji ana thamani, aliipata nasi. Amekuwa kwa kiwango kikubwa. Kila mtu anajua nini Dani Olmo anaweza kufanya. Kwa hiyo, kila mtu lazima awe wazi juu ya thamani yake na chini ya hali gani klabu inaweza kuwa tayari kuzungumza.

> ●●● Ana thamani, kila mtu anajua nini anaweza kufanya, hivyo klabu inaweza kuwa...

"Nadhani ni muhimu pia kwa Dani kuoneshwa thamani yake na kuijua. Na klabu ambayo inamtaka kabisa inapaswa pia kutenda haki kwa thamani ya Dani Olmo."

Mkataba wa Olmo na Leipzig ulijumuisha kifungu cha kuruhusiwa kuondoka cha euro milioni 60 ambacho kilimalizika mwezi uliopita.

Wakati Barcelona wanafurahia kulipa aina hiyo ya fedha, wababe hao wa Katalunya wanajaribu kufikia makubaliano ambayo yatawawezesha kufikia kiwango hicho kwa miaka kadhaa, huku Leipzig wakitafuta fedha nyingi haraka iwezekanavyo.

Mkurugenzi wa michezo wa Leipzig, Rouven Schroder, pia aliionya Barcelona kulipa ikiwa wanataka kweli kumsajili Olmo.

"Dani ana thamani ya ajabu kwetu - kama mchezaji na kama mtu," alisema.

"Hatuna shinikizo la kumuuza. Kwa jinsi mambo yalivyo leo, tunatarajia Dani kurejea kwetu baada ya likizo yake ya euro. Kila kitu kingine kinabaki kuonekana."

Rose amethibitisha hadharani nia yake ya kutaka kumbakisha Olmo msimu huu wa majira ya joto, wakati Mtendaji Mkuu wa Leipzig, Johann Plenge, aliipa hapo awali kutomuuza mchezaji yeyote.

## HABARI MICHEZO




# TEN HAG: SANCHO ATAANZA MSIMU KAMA MSHAMBULIAJI

**LOS ANGELES,** Marekani

ERIK ten Hag amependekeza kuwa Jadon Sancho anaweza kuanza msimu mpya kama mshambuliaji wa kati wa Manchester United ili kuziba nafasi ya Rasmus Hojlund ambaye ni majeruhi.

Hojlund atakosekana kwa wiki sita kutokana na jeraha la misuli ya paja alilolipata wakati wa mchezo wa kwanza wa ziara ya Marekani dhidi ya Arsenal.

Kwa kukosekana kwake, Sancho, aliyerejeshwa kikosini kutoka uhamisho wa miezi 10, aliwekwa namba tisa katika ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Real Betis Jumatano na kipigo cha 3-0 Jumamosi kutoka kwa Liverpool.

Na Ten Hag alisema anaweza kuanza katika safu ya mshambuliaji wa kati dhidi ya Manchester City wiki ijayo kwenye Ngao ya Jamii, na dhidi ya Fulham wikendi ya ufunguzi wa msimu wa Ligi Kuu England mbele ya mchezaji mpya, Joshua Zirkzee.

"Ndiyo, la sivyo tusingecheza naye pale," alisema Ten Hag alipoulizwa kama Sancho angeweza kuanza mbele dhidi ya Man City kwenye Uwanja wa Wembley.

"Hicho ndicho tunaweza kufanya ikiwa hatuna Rasmus, lakini bila shaka Joshua Zirkzee anaingia, ameanza mazoezi, lakini pia zingatia kwamba muda si mrefu kwenye mazoezi, hivyo basi kuchukua muda, na anatakiwa kuzoea soka la Uingereza na namna yetu ya uchezaji pia.

"Jadon ni mshambuliaji. Tunajua anaweza kucheza katika maeneo mengi."

Zirkzee, aliyesajiliwa kwa pauni milioni 36.5 kutoka Bologna, bado hajafanya mazoezi na kikosi baada ya kurejea Carrington kwa mapumziko yake ya kiangazi badala ya kujiunga na ziara ya Marekani.

Sancho, aliyerejea United baada ya kutumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo katika Klabu ya Borussia Dortmund, hajafunga bao la ushindani katika klabu hiyo tangu Mei 2023.

Marcus Rashford ni chaguo jingine la kuziba pengo la Hojlund, lakini Ten Hag alidokeza kuwa fowadi huyo wa Uingereza atasalia katika nafasi yake ya kawaida upande wa kushoto.

"Nadhani Marcus amefanya hivyo alicheza kama mshambuliaji hapo awali na anaweza kufanya hivyo, na hakika ni chaguo," alisema Ten Hag.

# Guardiola ajibu uvumi wa kuinoa England



**LOS ANGELES,** Marekani

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amejitenga na ripoti zinazomhusisha na kibarua kilichoachwa wazi cha kuinoa England.

Gareth Southgate alijiuzulu kama Kocha wa 'Simba Watatu' hao na hivyo kuhitimisha kipindi cha miaka nane cha usukani.

Wakati huo, aliiongoza timu hiyo kwenye fainali mbili Ulaya ingawa walifungwa na pia nusu fainali ya kwanza ya Kombe la Dunia katika kipindi cha miaka 28.

Miongoni mwa wagombea wanaotajwa kuzingatiwa na FA ni Guardiola, ambaye anaingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na City.

Lakini kabla ya mechi ya kirafiki ya Man City ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Chelsea nchini Marekani, Guardiola alisisitiza kuwa ana furaha katika Uwanja wa Etihad.

"Nipo hapa, nimefurahishwa sana. Siwezi kusema chochote. Sijui imetoka wapi. Nimeridhika sana hapa," alisema.

"Ninatamani sana wakati wachezaji wako tayari kurejea kuanza kufanya mazoezi wote pamoja na kujiburudisha kile tunachopaswa kufanya."

Ingawa Guardiola amebakiza chini ya miezi 12 kukamilisha mkataba wake uliopo City, hivi majuzi alifafanua kwamba hii haimaanishi kuwa muda wake katika klabu hiyo unafikia kikomo na bado anaweza kusaini mkataba mpya.

Zaidi ya Guardiola, kocha wa zamani wa Liverpool, Jurgen Klopp pia amepuuza mazungumzo ya kuchukua nafasi ya Southgate.

Mgombea anayeongoza Eddie Howe amezungumzia furaha yake ndani ya Newcastle United, ingawa alisisitiza alitaka uhakikisho wa jukumu lake kusonga mbele ikiwa atabaki St James' Park.

Wagombea wengine wa nafasi hiyo wanaaminika kuwa Graham Potter, Mauricio Pochettino na Lee Carsley, huku pia wakiwamo Sean Dyche na Thomas Frank.

# Arsenal yamuuza Rowe Fulham




**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imemuuza aliyekuwa mchezaji wao, Emile Smith Rowe kwenda Fulham.

Fulham imetoa kitita cha pauni milioni 34, ada ambayo imeweka rekodi ya kuwa mchezaji aliyesajiliwa kwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo.

Klabu hiyo imetoa pauni milioni 27 na nyingine milioni 7 kwa mchezaji huyo ambaye anaweza kuichezea klabu hiyo mchezo wake wa kwanza leo, Jumatatu katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Sevilla. Smith Rowe aliondoka katika kambi ya Arsenal mapema wiki hii na kwenda kukamilisha vipimo kisha akajiunga na kikosi cha Fulham kilichopo nchini Ureno.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ameichezea Arsenal michezo 25 tu tangu Agosti 2022 baada ya kutokuwa na nafasi katika kikosi hicho kinachonolewa na Mikel Arteta.

'Washika Mtutu wa London' hao wanamwachia kiungo huyo wakiwa wametoka kukamilisha usajili wa beki Riccardo Calafiori na sasa wanamfukuzia kiungo wa Real Sociedad na Hispania, Mikel Merino.

Uuzwaji wa Smith Rowe ni wa fedha nyingi zaidi kwa Arsenal toka walipomuuza Alex Oxlade-Chamberlain kwenda Liverpool mwaka 2017.

HABARI MICHEZO

## Wananchiii, Biashara kamili

INATOKA UKURASA 24

Pia ilikuwa ni mechi ya nne ya kirafiki kucheza kabla ya kucheza na Simba katika mchezo wa Ngao ya Jamii Alhamisi wiki hii.

Mechi zingine zilizocheza ni dhidi ya FC Augsburg ya Ujerumani ambapo ilifungwa mabao 2-1, ikashinda dhidi ya timu mbili za Afrika Kusini; TS Galaxy bao 1-0, kabla ya kuisulubu Kaizer Chiefs mabao 4-0.

## Fadlu: Tupo tayari kwa Dabi Alhamisi

INATOKA UKURASA 24

shughuli na ziara za kikazi, ingawa hata hivyo haikumzuia kuangalia tamasha hilo kwenye televisheni.

"Nawashukuru sana, nimerudi ziara sasa hivi nimefungua TV nimeona uwanja umejaa na shughuli zinaendelea. Nakumbuka mwaka jana tulikuwa sote hapo, lakini mwaka huu, limenipita lakini nikaona lisinipite kabisa kabisa mpaka niongee nanyi," alisema Rais Samia, ambaye alikuwa anasikika kupitia simu ya Msigwa na kushangiliwa na maelfu ya watazamaji waliokuwa uwanjani hapo.

Katika mechi hiyo, Simba iliichapa APR ya Rwanda mabao 2-0, yaliyowekwa wavuni na Debora Fernandes Mavambo kwa shuti kali la mbali, na Edwin Balua kwa mkwaju wa faulo, baada ya Valentino Mashaka kuangushwa nje kidogo ya eneo la hatari.

Mara baada ya mchezo huo, Kocha wa Simba, Fadlu, alisema sasa akili yake anaielekeza kwenye mchezo wa Alhamisi dhidi ya Yanga, akisema amewatazama wapinzani wake katika michezo kadhaa waliyocheza nchini Afrika Kusini.

"Tulikuwa na wiki nne za maandalizi, ingawa bado wachezaji wangu miguu ni mizito kutokana na mazoezi magumu waliyokuwa wakiyafanya, lakini bado haiondoi ukweli kuwa tunakabiliana na mechi ngumu na tuko tayari kwa dabi, nimeiona Yanga ikicheza mechi zake Afrika Kusini, hivyo tunakwenda kujiandaa," alisema.

Akizungumzia mchezo wa juzi, alisema kipindi cha kwanza hakikuwa kizuri sana kutokana na jinsi wachezaji wake walivyokuwa wakicheza, lakini alifurahishwa na kile alichokiona kipindi cha pili.

"Kipindi cha kwanza tulicheza pasi za taratibu, halafu ni nyingi bila kufanya mashambulizi haraka langoni mwa mpinzani, kipindi cha pili baada ya kuwaelekeza wachezaji wangu kwamba nini tunatakiwa tufanye, kuondoka na mpira haraka, kushambulia, kuwaweka wapinzani kwenye presha na ndicho tulichofanya," alisema raia huyo wa Afrika Kusini.

# AZAM YAIFUNZA SOKA RAYON NA ROBERTINHO

**Na Adam Fungamwangwo**

BAO la dakika ya 57 lililofungwa na beki Lusajo Mwaikenda, liliipa timu ya Azam FC ushindi wa 1-0 dhidi ya Rayon Sport katika mechi maalum ya kimataifa ya kirafiki iliyochezwa juzi katika Uwanja wa Pele, Kigali nchini Rwanda.

Timu zote mbili ziliitumia mechi hiyo kutambulisha wachezaji wake wa msimu mpya, ambapo Azam iliita tamasha hilo Azamka, na wenyeji walilipa jina la Rayon Sport Day, ambapo kabla ya mechi kulikuwa na burudani kadhaa.

**Kocha Robert Oliveira maarufu kwa jina la Robertinho, alionekana kwa mara ya kwanza akiifundisha timu hiyo, baada ya kuondoka Simba mwanzoni mwa Januari mwaka jana.**

Pia katika mechi hiyo, ilishuhudiwa kiungo mshambuliaji wa Yanga, Haruna Niyonzima, akiichezea timu ya Rayon.

Kocha wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema ilikuwa ni mechi nzuri ambayo imewapa kipimo tosha kuelekea kwenye mchezo wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya APR utakaochezwa Agosti 23 hadi 25, mwaka huu nchini humo.

"Ilikuwa mechi nzuri na kuna wakati ilikuwa ngumu sana kwetu, lakini ilikuwa ni jambo jema kupata mchezo kama huu kwa sababu ilikuwa ni muhimu kuja hapa kusoma mazingira ambayo yatatusaidia kwenye mechi yetu inayokuja dhidi ya APR, Ligi ya Mabingwa Afrika, na kiwango kilikuwa kizuri tu.

"Umeona uwanja mzima ulikuwa unaisapoti Rayon Sport, hata hivyo wachezaji wangu hawakujali na hii imetupa kujiamini katika mchezo wetu unaokuja," alisema Dabo.

Kwa upande wa Robertinho, alisema ndiyo kwanza ana siku tano tangu aitwae timu hiyo, akiahidi kufanya marekebisho ingawa kikosi chake kilicheza vema.

"Nimeanza kazi siku tano tu zilizopita, lakini wachezaji wangu wamepambana nawapongeza, kipindi cha kwanza tumecheza vema, kipindi cha pili pia, lakini tukajisahau ndani ya boksi tukafungwa bao," alisema raia huyo wa Brazil.




Kiungo wa Simba, Debora Fernandes Mavambo, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 2-0 dhidi ya APR ya Rwanda kwenye mechi ya Tamasha la Simba Day, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. Bao la pili lilifungwa na Edwin Balua. **MPIGAPICHA WETU**

## *Uhamiaji FC, Coastal kujipima kuelekea CAF*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Uhamiaji FC itacheza mchezo wake wa kirafiki dhidi ya Coastal Union kutoka Tanzania Bara kujiandaa na msimu mpya na mechi za kimataifa, imeelezwa.

Mchezo huo una umuhimu kwa timu zote mbili katika kuelekea mashindano ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ambayo yataanza kutimua vumbi baadaye mwezi huu.

Uhamiaji FC ni wawakilishi wa Zanzibar katika Kombe la Shirikisho barani Afrika wakati Costal Union nayo ikiiwakilisha Tanzania kwenye michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Afisa Habari wa Uhamiaji FC, Mwinyi Hamadi, alisema mchezo huo ni moja ya michezo ya kirafiki katika kuangalia kikosi chao kuelekea mchezo uliopo mbele yao.

Alisema mchezo huo wanaupa uzito kiuchezaji kwa kuwa wanacheza na timu ambayo hawapo katika ligi moja na inawachezaji wenye mbinu na uzoefu mkubwa. Alisema kupata mechi hiyo ya kirafiki ni mafanikio makubwa katika mpango wao kwa upande wa maandalizi kabla ya kuivaa Al Ahli Tripoli ya Libya.

"Mchezo huu si wa ushindani kwamba lazima tushinde, ni wa kujipima kwa kile ambacho wachezaji walichokipata kutoka kwa mwalimu, pia mwalimu atapata muda wa kukiangalia kikosi chake kuanzia mchezaji mmoja mmoja kwa nafasi yake," alisema.

Alisema kupitia mchezo huo anaamini wachezaji watapata nafasi ya kujifunza mbinu mpya, lakini pia kwa mwalimu atapata taswira halisi ya kikosi chake.

Aidha, alisema mpaka sasa timu hiyo imeonesha kiwango kizuri kupitia michezo mbalimbali ya kirafiki waliyocheza na timu za Zanzibar.

# Michezo

Jumatatu Agosti 5, 2024

Nipashe




Arsenal yamuuza Smith Rowe Fulham UKURASA 22



Mashabiki wa Yanga waliohudhuria Kilele cha Wiki ya Mwananchi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wananchiii, Biashara kamili Ngao ya Jamii

## Tamasha babkubwa lafana kwa Mkapa, huku wenyewe wakitamba...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Klabu ya Yanga jana ikifanya tamasha lake la sita la Kilele cha Wiki ya Mwananchi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, lililohitimishwa kwa mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Mabingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Red Arrows kutoka Zambia, gumzo kubwa sasa imekuwa ni mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii, Alhamisi wiki hii dhidi ya watani wao wa jadi, Simba.

Timu hizo zitakutana katika mechi ya nusu fainali itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na mshindi atakutana na timu itakayoshinda kati ya Azam FC na Coastal Union kwenye nusu fainali kwanza itakayopigwa siku hiyo hiyo Uwanja wa New Amaan Complex visiwani Zanzibar.

**Mashabiki wa timu hizo kila upande unaamini unaweza kufanya vizuri, hii ikiwa ni baada ya Simba kuonesha kiwango cha hali ya juu kwenye Tamasha la Simba Day dhidi ya APR ya Rwanda ambapo ilishinda mabao 2-0 uwanjani hapo juzi.**

Mashabiki hao wamekuwa wakisema sasa "bado Alhamisi" kila upande ukiamini wanaweza kupata matokeo.

Kabla ya mechi ya jana kati ya Yanga na Rayon Sports, wanachama na mashabiki wa timu hiyo walijitokeza kwa wingi uwanjani, ambako kulikuwa na burudani mbalimbali kutoka kwa wasanii wengi maarufu nchini.

Baadhi ya wasanii walipanda jukwaani kutumbuiza ni pamoja na Christian Bella, Harmonize, Meja Kunta, Billnass, Marioo, Diamond Platinum na wengineo.

Tamasha hilo limefanyika siku moja tu baada ya watani zao wa jadi Simba kufanya tamasha lao la 16 kwenye uwanja huo.

Mara baada ya burudani mbalimbali, kikosi cha Yanga cha msimu wa 2024/25 kilitangazwa, huku kikiwa na wachezaji wapya kwenye timu hiyo, lakini si wapya kwenye soka la Tanzania.

Wachezaji hao ni Clatous Chama aliyesajiliwa kutoka Simba, Prince Dube kutoka Azam FC, Duke Abuya kutoka Singida Black Stars, Aziz Andambwile, akitokea Singida Fountain Gate na wengineo.

Lilikuwa ni tamasha la sita kufanywa na klabu hiyo, ambapo lilifanyika mara ya kwanza 2019 ikicheza dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya, na kutoka sare ya bao 1-1.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo kukiona kikosi chao laivu, ambapo ilikuwa ikikishuhudia kwenye luninga kilipokuwa nchini Afrika Kusini katika michezo maalum ya kirafiki ya kimataifa.

INAENDELEA UKURASA 23

# Fadlu: Tupo tayari kwa Dabi Alhamisi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan, akiwataka wanachama na mashabiki wa Simba kusahau yaliyopita na sasa kuganga yajayo, Kocha Mkuu Fadlu Davils, amesema baada ya mechi ya juzi dhidi ya APR sasa wapo tayari kwa Dabi ya Kariakoo dhidi ya Yanga, Alhamisi ijayo kwenye Ngao ya Jamii.

Akizungumza juzi wakati wa Tamasha la Simba Day kupitia simu ya mkononi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, Rais Samia aliusalimia umati wa mashabiki zaidi ya 60,000 uliofurika Uwanja wa Benjamin Mkapa, akiwataka kusahau yote yaliyopita na kuangalia nini watafanya kwa msimu huu.

Msimu uliopita, timu ya Simba haikufanya vema kwenye michuano mbalimbali, ikiishia njiani kwenye Kombe la FA, pamoja na kumaliza nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu, ambayo imewanyima tiketi ya kwenda Ligi ya Mabingwa na badala yake msimu ujao itacheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Katika salamu zake hizo, rais ambaye mwaka jana alikuwa mgeni rasmi kwenye Simba Day huku mwaka huu akisema ameshindwa kuhudhuria kutokana na

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >

# Elimu nishati safi ya kupikia yatolewa shuleni

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

TAASISI ya Mazingira na Maliasili imeanza kutembelea shule na kutoa elimu ya kutumia nishati safi kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira.

Taasisi hiyo mbali ya kuzunguka katika shule, pia imejipanga kufikia jamii moja kwa moja na kutoa elimu kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Mwanawetu Saidi aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati yake ya kuleta mabadiliko kwenye matumizi ya nishati.

Mwanawetu alisema kuwa tayari wameanza kutembelea shule za serikali na binafsi kutoa elimu ya matumizi ya nishati mbadala huku wakijinasibu kujitolea mchango wao wa namna ya kutekeleza azimio hilo ili chakula kipikwe kwa nishati safi isiyoharibu mazingira.

"Tunataka kila taasisi iungane na Rais Samia Suluhu Hassan katika uhamasishaji matumizi ya nishati mbadala ya kupikia ikizingatiwa shule zetu nyingi zinatumia kuni na mkaa. Tutatoa mafunzo ya moja kwa moja na kujitolea ujuzi wetu ili kufanikisha azma ya utunzaji mazingira," alisema.

Kiongozi huyo alisema mbali ya kufika shuleni, pia watawafikia wavuvi na kutoa elimu bora ya uvuvi ambao hautaathiri mazalia baharini na viumbe wengine sambamba na kutunza mazingira pembezoni mwa bahari na vyanzo vya maji.

Mwalimu wa Shule ya Mount Calvary, Erick Kilonzo alisema tayari wameanza kuandaa jiko maalum litakalotumia nishati mbadala kupikia.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke Sixtus Mapunda (wa pili kulia) akikata utepe katika makabidhiano rasmi ya mradi wa Maji uliopo Mtaa wa Njaro, Wilaya ya Temeke ambao umekarabatiwa na Kampuni ya Sigara Tanzania na utawanufaisha zaidi ya wananchi 5000 wa eneo hilo. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa TCC Plc, Takashi Araki (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano, Patricia Mhondo na Diwani Viti Maalumu Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Caroline Henrich. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji kufundishwa kuandaa supu ya kitoga

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Mji Ifakara, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro inakusudia kutoa elimu kwa wafugaji samaki kutumia mabwawa ya asili na namna ya ukaushaji na uandaaji supu ya samaki, akiwamo kitoga.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji huo, Zahara Michuzi aliyasema hayo mjini Morogoro mwishoni mwa wiki alipotembelea na kukagua vipando katika eneo la Banda la Halmashauri hiyo katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere.

Viwanja hivyo ndiko yanakofanyika Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki inayojumuisha mikoa ya Morogoro, Pwani, Tanga na Dar es Salaam.

Mkurugenzi huyo alisema halmashauri hiyo imejipanga kutekeleza kauli ya Tanzania ya Kilimo kwa vitendo katika sekta ya kilimo, yakiwamo mazao ya kimkakati, mifugo na uvuvi.

Alisema kuwa kwenye ufugaji samaki, halmashauri hiyo imeandaa bwawa maalum la asili ili kuonesha teknolojia ya ufugaji samaki aina ya kitoga kwa njia ya asili.

Samaki hao wamekuwa na soko la uhakika nchini kutokana na kitoweo chao kupenda na watu wengi.

Alisema halmashauri hiyo imekuwa na mito mingi yenye samaki wengi wa aina, wakiwamo perege, njege, kitoga, njugu, kambare na wengineo ambao wanakubalika katika masoko nchini.

Alisema kuwa lengo la kuchimbwa bwawa la asili kwenye maonesho hayo ni kutoa fursa kwa wananchi wajifunze na kuhamasika kufuga samaki wakiwamo kitoga.

Alisema hatua hiyo ni sehemu ya mikakati ambayo halmashauri imejipanga kuwaonesha Watanzania na wana Morogoro; kwamba inajivunia kuwapo samaki na teknolojia rafiki na ya asili kwenye ukaushaji bora wa samaki.

Zahara alisema wataalamu wa sekta ya mifugo wamejipanga kutoa elimu ya ufugaji kwa wafugaji ili wawe na ubora katika ushindani wa soko na bei kubwa na yenye tija.

Alisema wataalamu wa kilimo pia watahamasisha kilimo cha mboga na matunda ili kuboresha afya za wananchi na wajipatie fedha.

Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Dk Yuda Mgeni, alisema halmashauri imejipanga kuonesha teknolojia mbalimbali za kilimo, ufugaji na uvuvi ikiwa ni pamoja na utoaji elimu kwenye sekta hizo.

Dk. Mgeni alisema licha ya maeneo ya Ifakara na Bonde la Kilombero kusifika kwa uzalishaji mpunga, kutokana na mazingira ya kuwapo mito ya asili, maeneo hayo pia ni maarufu kwa uvuvi.

"Kupitia maonesho haya ya Nanenane, tunamleta samaki aina ya kitoga ili kuwaonesha watu wamjue ubora wake na soko lake kwa ujumla. Wengi hawajawahi kumwona akiwa hai," alisema Dk. Mgeni.


## WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS

6th Floor, Golden - Jubilee Tower
7 Ohio Street/ Kibo Street
P.O. B OX 5119
11481 Dar - Es Salaam - Tanzania

Tel : +255 22 2922211
Fax : +255 22 2922211
E-mail: info@whi.go.tz
Website: www.whi.go.tz

FAIDA FUND

**TAARIFA YA MKUTANO WA KWANZA WA MWAKA WA WAWEKEZAJI KATIKA MFUKO WA FAIDA UNIT TRUST FUND ( FAIDA FUND)**

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano wa Kwanza wa Mwaka wa **FAIDA UNIT TRUST FUND** ('Faida Fund') utafanyika tarehe **10 Agosti, 2024** katika Kituo cha Mikutano Cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam kuanzia saa 2:30 asubuhi

Ajenda za Mkutano ni kama ifuatavyo:-

1. Kufungua Mkutano;
2. Kupitisha Ajenda;
3. Kupokea na Kuidhinisha Taarifa za Fedha Zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia Juni, 2023;
4. Taarifa ya Uwekezaji kutoka kwa Meneja Wa Mfuko;
5. Mengineyo ambayo taarifa zake zimewasilishwa kwa Msimamizi wa Mfuko;
6. Kufunga Mkutano.

**Zingatia:**

*1. Wawekezaji watakaohudhuria mkutano wanapaswa kuwa na Kitambulisho kama (kitambulisho cha taifa, kadi ya mpiga kura, leseni ya udereva, pasipoti, n.k.) kwa madhumuni ya usajili.*

*2. Nyaraka za Mkutano zinaweza kuchukuliwa kwenye Jengo la Golden Jubilee ghorofa ya 6 kuanzia tarehe 6 Agosti 2024 na pia zitapatikana kwenye tovuti ya Meneja wa Mfuko **www.whi.go.tz***

*3. Mwekezaji anaweza kumteua mwakilishi kwa kutumia fomu inayoweza kupakuliwa kutoka **www.whi.go.tz***

*4. Mengineyo katika kipengele cha 5 hapo juu itapaswa kumfikia Meneja wa Mfuko kabla ya tarehe 10 Agosti, 2024 kupitia namba ya simu 022 2922211 au S.L.P 5119 au **info@whi.go.tz** au **wekeza@whi.go.tz***

*5. Mwekezaji/Mshiriki wa mkutano huu atajigharamia mwenyewe.*

**Kwa niaba ya WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS**
**(Meneja wa Mfuko)**

**Dr Fred Msemwa**
**Mkurugenzi Mtendaji**

**11 Julai, 2024**


# Mmiliki mabasi ya Sauli afariki ajalini

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

MMILIKI wa mabasi ya Sauli, Sauli Solomon (40), amefariki dunia kutokana na ajali iliyotokea jana eneo ya Mlandizi, wilayani Kibaha, mkoani Pwani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea saa 12:30 asubuhi katika eneo la mteremko mjini Mlandizi.

Kwa mujibu wa Kamanda Lutumo, Sauli aliyekuwa anaendesha gari aina ya Jip, alipofika kwenye mteremko huo, lori lililokuwa nyuma lilimgonga kwa nyuma kisha gari lake kugonga lori lingine lililokuwa mbele na hivyo kubanwa katikati.

Inadaiwa Sauli alifariki dunia katika ajali hiyo huku mwanawe wa miaka minne ambaye alikuwa katika gari hiyo, akijeruhiwa. Alipatiwa matibabu na kuruhusiwa.



# Wakulima, wafugaji Meru waanzisha umoja

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKULIMA na wafugaji katika Wilaya ya Meru wameanzisha Umoja wa Wafugaji na Wakulima Meru (UWAWAME), kwa lengo la kuongeza mazao thamani.

Pia, wameanzisha viwanda mbalimbali vya kuchakata mazao ya mifugo na kilimo.

Akizindua umoja huo wilayani Arumeru kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, mbunge wa Arumeru Mashariki, John Pallangyo, alisema uzinduzi wa umoja huo una manufaa makubwa kwa wakulima na wafugaji hao.

Alisema watafanya shughuli zao kwa kushirikiana pamoja na kuanzisha miradi mikubwa itakayoleta tija kwao.

Alisema uwepo wa umoja huo pia utasaidia wakulima kuachana na kilimo na ufugaji usiokuwa na tija na hatimaye kuzalisha kisasa kupitia elimu watakayoipata ya mashamba darasa, itakayotolewa mara kwa mara na wataalamu waliobobea.

“Kwa kweli umoja huu ni muhimu sana kwa maslahi mapana ya wilaya yetu, kwani wakiungana na kuwa kitu kimoja watafanya mambo makubwa ambayo yatailetea halmashauri mafanikio na hata wakulima kuwa na uhakika wa soko,”alisema.

Mwenyekiti wa umoja huo, Jeremiah Kaaya, alisema asilimia 60 ya wakazi wa Halmashauri ya Meru ni wafugaji, kwamba kuna wafugaji 61,280 na mifugo mbalimbali.

Alisema: “Kwa sasa uzalishaji wa maziwa ni wastani wa lita nane hadi 12 kwa ng’ombe mmoja kwa siku, idadi ya ng’ombe wa maziwa ni 59,641 na ng’ombe wa nyama 32,745, wastani wa uzalishaji wa maziwa ni lita 7,800,000 hadi 12,000,000 kwa mwezi”.

Aliema mbali na umoja huo kuwa na malengo ya kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo pia wana matarajio ya kuwa na mashine ya kutotoa vifaranga, ili kuinua thamani ya mazao yanayozalishwa na kuipatia halmashauri mapato na ajira kwa vijana.

Kaaya alisema malighafi itakayotumika kwenye viwanda hivyo itazalishwa na wakulima kwani maziwa yatakwenda katika kiwanda cha kuchakata maziwa na mazao ya nafaka jamii ya mikunde yatauzwa katika kiwanda cha kuchakata vyakula vya mifugo.



Mkuu wa wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Fakii Lulandala (katikati) akizungumza kwenye kikao na wajumbe wa eneo tengefu la Mirerani kuhusu changamoto zinazowakabili wachimbaji wa madini ya Tanzanite juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wasomi, watafiti waimarisha nguvu kufikia SDG

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

RAIS wa ushirikiano wa kimataifa wa masuala ya ushirika-Kanda ya Africa (ICA), Tajudeen Ayeola, amesema wasomi na watafiti kutoka maeneo mbalimbali duniani wamechunguza na kuimarisha nguvu ya ushirikiano katika kufikia maendeleo endelevu Afrika.

Amesema mitazamo tofauti na mawazo ya kibunifu yaliyojadiliwa na wanazuoni hao siyo tu yameboresha uelewa wao kuhusu vyama vya ushirika na majukumu yao katika maendeleo endelevu, lakini pia yamesisitiza umuhimu wa kufanya kazi pamoja katika taaluma, sekta na mipaka ya kijiografia.

Chifu Ayeola, alieleza hayo mwishoni mwa wiki katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro alipokwenda kufunga mkutano wa kimataifa wa ushirika na maendeleo endelevu, ulioandaliwa na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na Chuo Kikuu cha Ushirika cha Kenya (CUK).

“Majadiliano yetu yamesisitiza kuwa maendeleo endelevu, si jambo la pekee bali ni dhamira ya pamoja. Vyama vya ushirika ni vyombo vyenye nguvu kwa maendeleo endelevu. Zinajumuisha kanuni za hatua ya pamoja na manufaa ya pande zote, ambazo ni muhimu kwa kushughulikia changamoto za wakati wetu. “Kwa kukuza ukuaji wa uchumi, ushirikishwaji wa kijamii na ulinzi wa mazingira; vyama vya ushirika vinaongoza njia kuelekea mustakabali endelevu na wenye usawa.” Alisema.

Alisema matokeo ya mkutano huo yatachapishwa na kusambazwa kwa wasomi, vyuo vikuu vya ushirika na kwa watunga sera kwa utekelezaji zaidi.

Pia, aliwataka waandaaji kutumia nafasi yao ya kipekee kuwashawishi watunga sera kutumia nguvu za vyama vya ushirika kwa maendeleo endelevu.

“Mkutano huu pamoja na mambo mengine, uliangalia jukumu kuu la vyama vya ushirika katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Vyama vya ushirika vinakuza ushirikishwaji; kuwakumbatia wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu,” alisema.

Mwaka 2014, Shirika la Kazi Duniani (ILO), lilibainisha vyama vya ushirika kuwa muhimu katika kukomesha umaskini, kuwawezesha wanawake, kutoa elimu bora, kuhakikisha afya, usalama wa chakula, nishati endelevu, kutengeneza ajira na ukuaji wa usawa.

Aidha, alieleza kuwa ajenda ya Umoja wa Mataifa (UN) ya mwaka 2030, inatambua jukumu muhimu la sekta binafsi, hasa vyama vya ushirika; kuwataka kuongeza ubunifu ili kukabiliana na changamoto za maendeleo endelevu.

Alisema kuanzia mwaka 2017 hadi 2023, UN ilipanua wigo wa vyama vya ushirika kujumuisha ujenzi wa amani, kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, kutokomeza umaskini, usalama wa chakula na kushughulikia majanga ya kimataifa kama vile milipuko na migogoro.

Alisema: “Kwa hiyo, ninawahimiza wasomi wetu kuendelea na utafiti unaofahamisha sera na maamuzi kuhusu maendeleo ya ushirika.”

# Mradi kunufaisha wakazi 20,000 Hanang’

**Na Beatrice Shayo,** HANANG

SHIRIKA la WaterAid limekabidhi mradi wa uboreshaji wa huduma za miondombinu ya maji na usafi wa mazingira Wilaya ya Hanang’ mkoani Manyara uliogharimu Sh. milioni 425 na unalenga kuwafikia wanufaika wasiopungua 20,036.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkaazi wa shirika hilo, Ana Mzinga, wakati wa hafla ya makabidhiano ya mradi huo katika Kijiji cha Bashang na Laghanga vilivyopo katika Wilaya ya Hanang uliokamilika ndani ya mwaka mmoja, chini ya ufadhili wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Mzinga alisema Septemba Mwaka 2023 walifanikiwa kuzindua utekelezaji wa mradi huo mjini Katesh katika kikao cha wadau, kwa sasa umekamilika na wananchi kuanza kunufaika.

Aidha, alisema katika kikao hicho yapo mengi yaliwasilishwa na kujadiliwa, kubwa lililobaki kwao kama taasisi lilikuwa lile la kuahidiwa ushirikiano wa dhati wa kitendaji, ushauri wa kiuongozi na ulinzi katika kutekeleza mradi huu.

Mzinga alisema Shirika la WaterAid, ni taasisi isiyo ya kiserikali inayotekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na serikali ili kufikia watu katika maeneo mbalimbali ulimwenguni kwa huduma ya maji safi na salama, vyoo bora na mazingira salama ya usafi na usafi binafsi.

Meneja Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki, Leah Kaguara, alisema WaterAid inafanya kazi kwa kushirikiana na serikali kuhakikisha kuwa kila mtu anafikiwa na huduma za maji salama, usafi wa mazingira na usafi.

Alisema WaterAid ilizindua mkakati wake mpya wa kimataifa mwaka 2022 na programu za nchi za Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na Tanzania zilitengeneza na kuzindua mikakati yao mwaka 2023.

“Lengo letu la kwanza katika mkakati huu kusaidia kupatikana kwa huduma za maji, usafi wa mazingira na usafi (WASH) ziwe endelevu inayojumuisha na salama. Huduma katika eneo la Wilaya ya Hanang kwa ajili ya mabadiliko mapana huku lengo la pili likilenga kuweka kipaumbele cha WASH katika sekta ya afya ili kuboresha afya ya umma,” alisema.

Alisema wataendelea kufanya kazi mjini Hanang ili kuunga mkono mipango ya serikali ambayo inalenga kuhakikisha kila mtu katika wilaya hiyo anakuwa na huduma endelevu zinazojumuisha WASH.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Athuman Likeyekeye, alishukuru kwa mradi huo na kueleza kuwa miundombinu yote iliyopangwa kutekelezwa imekamilika vizuri na ipo tayari kwa matumizi.

Alisema mradi huo utawanufaisha wananchi wa Kata ya Laghanga, Wareta na maeneo ya jirani wakiwemo wanafunzi, wagonjwa.